SUPA JACKPOT
TZS. 1,104,580,144
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#




**RC** ajitosa kujibu tuhuma nzito ufisadi alioibua Gambo

UKURASA 3


Ukurasa 12
'Kuchumbia mazao' na ujazo wa lumbesa unavyodhulumu jasho la mkulima shamba
Ukurasa 13
Maradhi ya bodaboda, daladala yanapoambukiza askari trafiki
BUFE
IJUMAA APRILI 21, 2023
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA
Ukurasa 14
Kahitimu sheria akaweka cheti pembeni, kazama kwenye ujasiriamali 'njia nyeupe'

UCHUMI

Mkataba alioshuhudia Samia, kupaisha uchumi mtaji wa madini Sh. trilioni 1.6

Na Mwandishi Wetu

• Neema ndani ya Songwe, Lindi, Ulanga...
• Lengo lake sekta itoe 10% GDP lakaribia

HADI sasa Tanzania ni nchi inayomiliki rasilimali nyingi zikiwamo madini ambayo yana uwezo mkubwa kukuza uchumi wake. Pia, hilo linaendana na uhalisia, kiongozi mkuu wa nchi, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, naye yuko ndani ya mstari huo akionyesha shauku ya kupeleka mbele gurudumu la maendeleo ya Watanzania, ikiwamo kutumia maslahi yao.

Hiyo inaendana na kuwapo rasilimali za kimsingi kitaifa zenye nafasi ya kuhamasisha mwamko wa uchumi kitaifa, kama vile ardhi safi na yenye rutuba, milima, bahari, mbuga za wanyama, zilizozagaa kila pembe ya nchi.

Tanzania hadi sasa imebahatika kuwa na ardhi kubwa na rasilimali zinazochochea uchumi wa nchi. Hapo ndani yake inajumuisha madini yanayotafutwa duniani, kwa ajili ya uzalishaji bidhaa mbalimbali.

Ikirejewa miaka miwili na ushee iliyopita wakati Rais Dk. Samia anapewa mikoba ya mtamgulizi wake, marehemu Rais, Dk. John Magufuli, aliamua kukuza na kuendeleza miradi ya kimkakati aliyokabidhiwa kuiendeleza, akiwa na shauku kuona nchi inapiga hatua kubwa za kiuchumi kwa kuboresha sekta ya madini.

Hadi sasa Tanzania imo katika maeneo yaliyobarikiwa kuwa na madini adimu kama vile dhahabu, tanzanite, chuma, nicol, shaba, ruby, almasi, chokaa, chumvi, gesi, uranium na makaa ya mawe, yakipatikana kwenye mikoa iliyobahatika kama vile: Lindi, Morogoro, Mara, Shinyanga, Tabora, na Songwe yakiwa na maeneo nyeti ya madini.

Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akishuhudia Waziri wa Madini, Doto Biteko na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Jaji Eliezer Feleshi, wakitia saini Mkataba wa Makubaliano ya Msingi kati ya serikali na kampuni ya uchimbaji madini Peak Rare Earth, ya Australia iliyowakilishwa na Mwenyekiti Mtendaji wake, Russell Scrimshaw wa pili (kulia) na Ofisa Mtendaji Mkuu wa kampuni hiyo, Bardin Davis, Ikulu Chamwino Mkoani Dodoma, Aprili 17 mwaka huu. **PICHA: MTANDAO**

Ni siku chache tu zimepita, Rais Dk. Samia amezungumza namna nchi inatarajiwa kwenda mbele ikisimamia sekta ya madini inayoongozwa na Waziri wake, Dotto Biteko, aliyepewa jukumu hilo tangu zama za mtangulizi, hayati Dk. Magufuli. Ni uwasilisho wake, wakati Rais anashuhudia utiaji saini mikataba ya uchimbaji madini ya kinywe kwa mikoa ya Lindi, Morogoro na Songwe.

Inaelezwa kuwa jambo la kuchochea mwamko wa uchumi nchini, hasa ikizingatiwa mikataba inayoangukia uwekezaji mkubwa inaletwa nchini na ina faida kubwa kutoka kwenye mauzo. Pia, hisa za serikali ndani ya uwekezaji wa miradi hiyo inapaa, jambo ambalo matokeo yake yanaangukia tafsiri ya kiuchumi, uwekezaji hisa nchini na uchumi kitaifa, unakuwa katika thamani ya juu; vyote vikiangaliwa vinabaki kuchangia kasi ya ukuaji uchumi kitaifa.

"Mikataba mipya iliyosainiwa na serikali italeta nchini mtaji wa Dola Milioni 667 (takriban Shilingi za Kitanzania Trilioni 1.6) katika kipindi hiki kigumu cha kiuchumi duniani na kuleta ahueni kwa nchi yetu. Mikataba yote hii ya madini ya kimkakati kupitia sisi na wenzetu kampuni tatu za nchini Australia, ni sehemu ya kuipaisha Tanzania katika ramani ya dunia, kwa kuangalia eneo lote la uchimbaji, uchakataji na usafirishaji kwenye mataifa makubwa yaliyoweka mkazo kwenye sekta hiyo kupitia nchi yetu," anasema Rais Dk. Samia.

Hadi sasa, zama za uongozi wa nchi unaoendelea Awamu ya Sita, mchango wa sekta madini kwenye pato la taifa umeongezeka kwa kiwango kikubwa. Hadi Desemba mwaka jana, inatajwa ilikuwa asilimia 9.7, ikikaribia lengo la Rais Dk. Samia asilimia 10 ya Pato la Taifa au zaidi, ifikapo mwaka 2025.

Ishara za kiuchumi zinaonyesha sekta hiyo kufanikiwa sana, kuvuka malengo yake. Pia, ni mkakati usio mbali na kuwalinda, pia kuwainua wachimbaji wadogo, ikibeba tafsiri ya kumwinua Mtanzania mmoja mmoja.

"Mchango kwa wachimbaji wadogo kwenye sekta hii umeongezeka maradufu, kufikia asilimia 40 chini ya uongozi wa Rais Samia, kutoka asilimia 20 aliyoikuta alipoingia madarakani" anasema Waziri Biteko na kuongeza: "Serikali itaendelea kuongeza uwezeshaji, ikiwamo kuongeza kasi katika michakato mbalimbali katika maeneo ya wachimbaji wadogo, ili watumie vifaa na nyenzo za kisasa kama njia ya kuongeza ufanisi kwenye sekta hii muhimu kwa nchi yetu."

Rais Dk. Samia anasema, uwekezaji huo tajwa, unaenda kwenye mikoa ambayo bado uchumi wake haujatengemaa sana, pia ni miradi inayoenda kuinua ukanda huo, kwa kufungua fursa na kuwanyanyua wananchi wa maeneo hayo kwa kasi kubwa, kupitia mnyororo wa thamani, hata kuacha musukumo changamoto kwa wakazi husika kuchangamkia fursa zinazojitokeza kwa ajili yao na taifa kwa jumla.

SAFARI YA MABORESHO

Kabla ya kufikia hatua iliyopo ya utiaji saini, suala la utafiti

INAENDELEA UK.14

UKURASA 11

# Nipashe

Ijumaa Aprili 21, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581287
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
LIKE & FOLLOW US

# Uchunguzi washika kasi mafunzo ya 'ushetani'

• **Ni** kwa walimu 244 walionaswa hotelini. Mkuu wa Mkoa, CWT wafunguka... *Endelea ukurasa 2*

## Kigogo mstaafu Bunge aiambia Tume Hakijinai rushwa imekithiri uteuzi wagombea ubunge, udiwani

UKURASA 4



Umati wa wananchi wakitafuta mahitaji mbalimbali ya Sikukuu ya Idd el Fitr katika Mtaa wa Kongo, Kariakoo jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Moshi wa jenereta ulivyowaua wanafamilia wanne usiku mnene

UKURASA 2





Kampuni ya the Guardian Limited, Wachapishaji wa Magazeti ya the Guardian na Nipashe, inawakaribisha wadau wote wa maendeleo kutoa salaam za pongezi wakati tunaadhimisha miaka 59 ya muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

Toleo hili litachapishwa tarehe 26 Aprili, 2023 kwenye Magazeti ya Guardian na Nipashe.

The Guardian    Nipashe

Kwa mawasiliano zaidi,
Tupigie +255 677 020 701

Email: advertise@guardian.co.tz or Visit us at The Guardian Limited, Mikocheni Light Industrial Area, Opposite ITV / Radio One, Dar es Salaam
Web: www.ippmedia.com / epaper.ippmedia.com

HABARI KITAIFA



Kaimu Kamanda wa Jeshi la Zimamoto na Ukoaji Mkoa wa Mwanza, SF Kamila Labani akikagua jiwe lililoleta taharuki kwa wakazi wa mtaa wa Mkapa, kata ya Igoma, jijini Mwanza juzi, baada ya kuanza kuhama kwenye eneo lake la asili likielekea katika makazi ya watu. Habari Uk. 10. **PICHA: VITUS AUDAX**

# Uchunguzi washika kasi tuhuma mafunzo 'ushetani'

**Na Mary Mosha, MOSHI**

SIKU chache baada ya uongozi wa Wilaya ya Same kusitisha mafunzo kwa walimu yaliyodaiwa kukiuka maadili ya kitanzania, Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu amesema wameongeza nguvu kuchunguza suala hilo.

Amesema Katibu Tawala wa Mkoa huo, Tixon Nzunda ni sehemu ya timu ya uchunguzi huo na jana alikuwa safarini kwenda wilayani Same kwa lengo la kushughulikia suala hilo.

Juzi, Nipashe iliripoti namna Kamati ya Ulinzi na Usalama Wilaya ya Same iliyolazimika kuingilia kati na kusitisha mafunzo hayo yaliyokuwa yanatolewa kwa walimu 244 na taasisi isiyo ya kiserikali (jina tunalo) baada ya kubaini dosari, ikiwamo vitabu vinavyotumika kufundishia kuwa na viashiria vya maadili yasiyofaa.

Mafunzo hayo yalikuwa yalikuwa yanatolewa kwa walimu wa shule za msingi na sekondari wilayani humo, yakipewa jina la 'Mafunzo ya Afya ya Jamii, Afya ya Uzazi na Uhusiano'.

Mkuu Mkoa (Babu), katika mazungumzo na Nipashe jana, alisema: "Kamati ya Usalama ya Mkoa tunalijua hilo suala, na Katibu ameondoka leo (jana) Aprili 20 kuelekea wilayani Same kwa ajili ya kufanyia kazi suala hilo.

"Nilisahau kumuuliza kama kuna tume yoyote imefika kwa ajili ya suala hilo ila kama ipo ni kawaida kwa utendaji wa kazi wa serikali.

"Mimi nilikuwa safari, nilirejea jana (juzi), hivyo tunalifanyia kazi jambo hili kwa mikakati ya siri na ya wazi na litakapokamilika, tutatoa taarifa," alifafanua Babu.

Mkuu wa Mkoa huyo alisema ni wajibu wa serikali kuhakikisha hakuna vitendo vya uvunjifu wa amani na ukiukwaji wa maadili, akitoa angalizo kwa watu wanaonung'unika kuwa walimu hao wameonewa, akisisitiza "waache mara moja".

Katika hilo, Babu alisema "Nimesikia kuna manung'uniko na malalamiko kwa baadhi ya walimu, wakiona walimu wale wameonewa, lakini niwaombe walimu wawe watulivu wakati Katibu Tawala wa Mkoa anashughulikia jambo hili na hakuna hata upande mmoja utakaoonewa.

"Lengo sio kumwonea mtu ila tunataka walimu wetu fursa nzuri zinapokuja, waweze kunufaika nazo, na wasinufaike na mambo mabaya yatakayokuja kuharibu watoto," alisema.

Kiongozi huyo wa mkoa pia aliyataka mashirika yasiyo ya kiserikali yaliyoko mkoani Kilimanjaro, kutii sheria zote, hasa wale wanaojihusisha na utoaji wa elimu kwa jamii na kuahidi kutolivumilia shirika lolote litakalovunja sheria.

"Ninaruadia, kuna vitabu ambavyo vimekatazwa na kupigwa marufuku na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na zipo baadhi ya NGO bado zinavitumia, Niwaombe kuacha mara moja na kufuata utaratibu. Wasipofuata utaratibu, hatutowavumilia," alionya.

**CWT WAFUNGUKA**

Akizungumzia suala hilo, Katibu wa Chama cha Walimu (CWT) Mkoa wa Kilimanjaro, Daudi Mafwili, alisema watatumia mifumo yao kuendelea kuongeza nguvu ya kutoa elimu kwa walimu ili kunusuru jamii ya kitanzania.

"Wanachama wetu wamekuwa wahanga (waathirika) wakubwa wa kila kitu kipya kinachokuja kwenye jamii hasa chenye maslahi, walikuja watu wa QNET na DECI na sasa wamekuja hawa jamaa wenye mambo yao, bado wanaonekana walimu ndio kundi kubwa la waathirika. Tutatumia vikao na makundi yetu kuendelea kutoa elimu kwa wanachama wetu.

"Ila hatutowavumilia wale wote serikali itakaobaini walishiriki jambo hili kwa nia ya kuharibu kizazi cha watanzania," Mafwili alihadharisha.

Mwezi Januari mwaka huu, Nipashe iliripoti kuhusu baadhi ya watendaji wa shule binafsi mkoani Kilimanjaro kuwafundisha kulawitiana wanafunzi, hasa wanaolala bweni. Serikali iliunda timu ya kuchunguza suala hilo.

# Moshi wa jenereta ulivyowaua wanafamilia wanne usiku mnene

**Na Jenifer Gilla**

WATU wanne wa familia moja wakazi wa Chang'ombe, wilayani Temeke jijini Dar es Salaam, wamefariki dunia baada ya kuvuta moshi wa jenereta walililoliwasha ndani ya nyumba yao.

Taarifa iliyotolewa jana kwa vyombo vya habari na Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, SACP Muliro Jumanne, ilisema kuwa Aprili 18, mwaka huu saa nne usiku watu hao waliwasha jenereta na kuliweka ndani ya nyumba baada ya umeme kukatika.

Iliwataja waliopoteza maisha kuwa ni Kazija Mohamed (21), Munir Ibrahim (7), Munira Ibrahim (6) Muyyat Ibrahim (3) huku Ibrahim Juma (28) na Aisha Ayubu (29) ambao ni mume na mke, hali zikielezwa kuwa sio nzuri na wanaendelea kupatiwa matibabu katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili.

Alisema jeshi hilo kwa kushirikiana na mamlaka nyingine linaendelea na uchunguzi baada wa awali kuonyesha watu hao walipoteza maisha baada ya kuvuta hewa inayodaiwa kuwa ni chafu iliyotokana na moshi uliotoka kwenye jenereta walilolisha ndani ya nyumba yao na kulala.

# Wanaoishi mabondeni nchini wapewa hadhari

**Na Faustine Feliciane**

WANANCHI wanaoishi katika maeneo ya mabondeni mikoa ya Dar es Salaam, Pwani na Zanzibar wamehadharishwa kuhusu mvua kubwa inayoendelea kunyesha kwenye mikoa hiyo.

Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA) kupitia taarifa yake ya juzi, imetoa hadhari ya mvua kubwa kwa mikoa ya Dar es Salaam na Pwani, pia baadhi ya maeneo ya Mkoa wa Morogoro na visiwa vya Pemba na Unguja.

TMA imetabiri uwezekano wa kunyesha mvua kubwa Dar es Salaam kwa siku mbili kuanzia kesho, ikitarajiwa hali kama hiyo mikoa ya Pwani na Morogoro.

Kaimu Mkurugenzi wa TMA, Dk. Ladislaus Chan'ga aliiambia Nipashe kuwa wananchi hususani wanaoishi mabondeni wanapaswa kuchukua tahadhari ya mvua hiyo.

Alisema kinachoendelea sasa ni utabiri walioutoa Februari 22 mwaka huu, waliposema kutakuwa na mvua za wastani mpaka chini ya wastani, kuwapo vipindi vya mvua kubwa katika mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, baadhi ya maeneo ya mikoa ya Morogoro, Pwani na Zanzibar.

"Tunaendelea kutoa angalizo kwa wananchi, wanapaswa kuchukua tahadhari katika kipindi hiki. Kama tulivyotabiri, Mkoa wa Dar es Salaam umeendelea kuwa na vipindi vya mvua kubwa, hivyo wananchi waishio kwenye maeneo hatarishi ni vyema wakachukua hatua," alisema Dk. Chang'a.

Alisema mvua hizo zinatarajiwa kuleta athari za kimazingira na uchumi kwa maeneo tajwa.

"Tunatarajia baadhi ya maeneo yatazungukwa na maji, na uharibifu wa miundombinu, hivyo kuathiri shughuli za kiuchumi," alisema Dk. Chang'a

Alisema kuwa TMA itaendelea kufuatilia mwenendo wa mifumo ya hali ya hewa na kutoa taarifa kwa wananchi ili kuendelea kuchukua tahadhari.

Tayari mvua hiyo imeanza kuleta madhara kwa baadhi ya maeneo nchini. Mkoani Mtwara, baadhi ya wananchi wamekosa makazi kutokana na nyumba kubomoka.

Mwishoni mwa wiki nyumba takrikan 600 mkoani Dar es Salaam ziliripotiwa kuzingirwa na maji na barabara ya Segera-Tanga ilikata mawasiliano kwa muda hadi pale Wakala wa Barabara (TANROADS) ulipochukua hatua kufanya matengenezo yaliyofanyika hadi usiku.

# RC ajitosa kujibu tuhuma za ufisadi alioibua Gambo

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

BAADA ya kuwa kimya kwa muda mrefu, Mkuu wa Mkoa wa Arusha, John Mongella, ameibuka na kujibu tuhuma za Mbunge wa Arusha Mjini, Mrisho Gambo, kuhusu ubadhirifu wa fedha unaodaiwa kuwapo katika Halmashauri ya Jiji la Arusha.

Akizungumza jana jijini hapa katika Wiki ya Maadhimisho ya Miaka 59 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar wakati wa uzinduzi wa madarasa manne yaliyojengwa kwa Sh. milioni 80 zilizotolewa na serikali kuu, kwenye Shule ya Sekondari Kaloleni, Mongella alisema hapendezwi na suala la ubadhirifu wa fedha za umma, lakini suala hilo liko katika mamlaka za kisheria.

Pia alitoa angalizo kwa huyo mtu (hakumtaja jina) anayetuhumu viongozi wa serikali ajitathimini kwa kuwa anaweza kuita wenzake wezi wakati na yeye ni mwizi lakini anajificha kwa kivuli cha kupita barabarani kila kukicha kusema wenzake.

"Hivi wewe ni mtu mzima unapita barabarani na mkeo anatokea mtu anamkonyeza mkeo, we utaacha kuendelea na safari umfuate anayemkonyeza mkeo? Unaachana naye maana ni lijinga liende zake. Sasa ukiacha safari yako ukamfuata huyu wewe ndio utaonekana lijinga.

"Viongozi wangu katika ngazi zote fanyeni kazi na nawapongeza mko katika njia sahihi ya kusimamia maendeleo.

Achananeni na mtu mmoja mjinga anayetaka muache dira yenu ya kusimamia miradi ya wananchi, mmfuate yeye mwenye maslahi yake binafsi. Asiwatoe barabarani mtaonekana wajinga kama huyu aliyeacha safari yake kumfuata aliyemkonyeza mkewe," alisema.

Aidha, alisema Jiji la Arusha kweli kulitokea ubadhirifu na kesi ipo mahakamani inaendelea, hivyo ni busara kuiachia sheria ichukue mkondo wake.

"Hakuna kushabikia ubadhirifu hapa kwa sababu tutapunja wananchi. Hata mimi Mongella nikifanya ubadhilifu lazima nitapambana na sheria. Lakini siwezi kutoka barabarani nikaanza wenzangu au watu wezi, wakati mwizi ni mimi mwenyewe.

"Mfano umefika pale Kariakoo unaweza kupigwa wakati wewe ndio uliyeibiwa. Kumbe mwizi anaondoka au ndiyo anayepiga kelele barabarani mwizi," alisema.

Pia alisema binafsi amejaliwa kukaa katika mfumo kwa muda mrefu lakini hajawahi kuona fedha nyingi za miradi ya maendeleo zikiletwa kwenye miradi kama katika serikali ya sasa.

Alisema kutokana na fedha hizo watendaji au wataalamu wake wana kazi za kufanya nyingi, kuhakikisha fedha hizo zinatekeleza miradi iliyokusudiwa na si kutoka barabarani kujibizana na anayepigia kelele wenzake wezi kwa maslahi yake binafsi atawasababishia mkwamo kwenye kazi.

"Arusha watu wake wanajua kuchagua pumba na mchele.Hatutekenyeki kirahisi, fanyeni kazi asitokee mtu wa kuwatoa katika reli. huwezi mnyooshea mwenzako kidole amejikojolea wakati wewe mwenyewe ndio kikojozi, fanyeni kazi Arusha ni salama na tulivu na kazi zinafanyika na kuonekana, tunamshukuru Rais Samia kwa kutumwagia fedha za miradi lukuki ya maendeleo,"alisema.

Mongella alisema matatizo duniani kote yapo na hayawezi kuisha na ndiyo maana viongozi wapo kwa ajili ya kuyatatua lakini si sababu ya kupita barabarani kunyooshea viongozi vidole kila kukicha kwa maslahi binafsi kuwa kuna matatizo.

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Arusha, Zelothe Steven, alisema wazazi sasa wamepumzika kuchangishwa fedha za ujenzi wa madarasa kwa sababu ya serikali kuwajali, hivyo si wakati wa kusikiliza maneno ya kuponda kuwa hakuna kazi inayofanyika yanayotolewa na mtu mwenye maslahi yake binafsi.

"Kazi kubwa zinafanyika na asitokee mtu akawaaminisha kwa maslahi yake binafsi na kuteka mambo ya chama akayafanya mambo yake. Hatuna mambo ya mtu binafsi,tupendane ,tuheshimiane na tusipimane, tuendeleze amani na utulivu kuujenga mkoa wetu wa utalii ambao unazidi kupaa,"alisema.

# Wabunge watoa mbinu kuepuka upendeleo ajira serikalini

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

WABUNGE wameitaka serikali kutoona haya kuiga na kuuchukua mfumo wa usaili wa ajira unaotumiwa na Mahakama nchini, wakiutaja ni bora katika kuhifadhi na kuchakata majina ya waombaji wa ajira kwenye kanzidata.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, Dk. Joseph Mhagama, wakati wa semina iliyoandaliwa na Tume ya Utumishi wa Mahakama kwa wajumbe wa kamati hiyo jijini hapa, alisema mfumo huo ukitumiwa na serikali, utasaidia kuepusha manung'uniko yanayosikika sasa kuhusu ajira serikalini.

Alisema kamati inapendekeza mfumo huo kutumiwa nchi nzima katika kipindi hiki, akifafanua kuwa wabunge wameonyesha kutoridhishwa na mfumo unaotumika sasa wa kuwasaili waombaji ajira, ikiwamo mchakato unaoendelea katika ajira za elimu na afya baada ya serikali kutangaza ajira 21,130.

"Huu mfumo ambao Tume ya Utumishi wa Mahakama imekuwa ikiutumia, hebu uwe kielelezo kwa taifa kwa wakati wote wanapotaka kuajiri watumishi wapya.

"Mfumo huu unaondoa shaka ya nani kaajiriwa kwanini. Ninadhani ndio itakuwa njia sahihi ya kupesha lawama na upendeleo kwenye utoaji wa ajira kwa wenye sifa.

"Jambo la kuangalia ni namna gani mfumo wenu unakuwa na usalama. Tukijiridhisha, basi kuna haja ya kuwaomba wenzetu TAMISEMI (Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa) waje kujifunza ili waanze mara moja kutumia mfumo huo kwani tumeshuhudia mara kadhaa mkitoa nafasi bila malalamiko," alisema Dk. Mhagama.

Alitoa angalizo kuwa serikali ikishindwa kuutumia mfumo huo, itazame njia nyingine kuliko inayotumika kwa sasa ambayo alisema inasababisha usumbufu na wabunge wanaona imepitwa na wakati kutokana na kuwalundika waombaji bila kujali gharama wanazozitumia.

Awali Mtendaji Mkuu wa Mahakama, Prof. Elisante Ole Gabriel alisema hawana tatizo kama serikali itahitaji kujua mfumo wanaotumia kusaili waombaji wa a jira, hivyo "tutatoa ushirikiano".

Prof. Ole Gabriel alisema kuwa ndani ya mahakama hawaiti kundi la watu, bali kila mmoja anasailiwa kutoka eneo lake na majibu anayapata papo hapo kama amechaguliwa au ameshindwa.

Alitolea mfano kuwa mwaka jana, walitangaza nafasi 215, lakini Watanzania walioomba walikuwa 15,432, akiwa na angalizo kwamba wasingekuwa na mfumo mzuri, ingekuwa kazi ngumu kuwaita pamoja na kuwafanyia usaili.

"Tulishajifungia na kuja na mfumo ambao una ulinzi wa kutosha kabisa, kila mtu alisailiwa akiwa mahali pake na alipata majibu hapo hapo, hii haina 'vimemo' wala kujuana, bali sifa ya mtu inampeleka kazini," alisema Prof. Ole Gabriel

Mtendaji huyo alisema waliutumia mfumo katika nafasi 400 za ajira za mahakimu, wakipokea maombi 2,000 huku nafasi 80 za makatibu mahtasi zikiombwa na watu 3,600.

Kuhusu malalamiko mahakamani, Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu Kanda ya Iringa, Elvin Mgeta alisema ni vigumu kumaliza malalamiko ikiwa tume za maadili hazitasimama kwenye nafasi yake.

Jaji Mgeta alisema mara nyingi watu wanabaki na malalamiko na manung'uniko bila kujua nini wakifanye, hivyo akaomba tume za maadili zilizo chini ya wakuu wa mikoa na wilaya, kusimama kwenye sehemu yake ili Jaji Mkuu naye asimamie kile kinachotakiwa.



HABARI KITAIFA




Msimamizi wa Huduma za Wateja na Masoko wa Benki ya DCB, Elizabeth Ntulu (kulia) na Ofisa Uhusiano wa benki hiyo, Dalila Issa (kushoto), wakikadhi sehemu ya madawati 30 yaliyotolewa na DCB kwa wanafunzi wa Shule ya Msingi Sandali kupitia kampeni yao ya "DCB Elimu Mpango Mzima na Mama Samia", Shuleni hapo, Temeke, Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kigogo mstaafu Bunge aiambia Tume Hakijinai rushwa imekithiri uteuzi wagombea wa ubunge

**Na Christina Mwakangale**

KATIBU wa Bunge Mstaafu, George Mlawa, amependekeza iundwe mahakama huru ambayo itashughulikia kesi za kisiasa, mashauri yanayohusu rushwa hasa kwenye mchakato wa upatikanaji wagombea ubunge na udiwani ndani ya vyama.

Amesema katika maeneo hayo, kumekithiri rushwa hususan kwenye vyama vikubwa kuanzia ngazi ya kuteua na kupitisha majina ya wagombea, jambo linarudisha nyuma maendeleo na kuminya haki ya mgombea na wananchi.

Akizungumza jana, jijini Dar es Salaam baada ya kutoa maoni yake mbele ya Tume ya Haki Jinai, Mlawa alisema kwa uzoefu wake, mbali na kuwapo Tume ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), kwenye majimbo na kata wagombea wanaoshinda kwa kiasi kikubwa hutumika rushwa.

"Uteuzi wa ubunge, wagombea wengine hata udiwani, kule kuna baadhi wagombea wanatoa rushwa. Nimekuwa Mbunge, nimeona. Sijui kwa vyama vidogo, ila kwa vikubwa hali ni hiyo.

"Wajumbe si watu wazuri, utakuta mgombea ana sifa nzuri tu, ila hapitishwi. Utakuta mgombea ana mnunulia mtu bodaboda anamjengea nyumba, ili ashinde," alisema Mlawa.

Mlawa ambaye aliwahi kuwa kwenye nafasi hiyo kwa takribani miaka tisa, alishika pia wadhifa wa Kamishna wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, kutumikia Ofisi ya Rais kuwa Mshauri wa Rais wa Katiba na Sheria pamoja na Naibu Katibu wa Tume ya Jaji Nyalali ya kukusanya maoni ya mfumo wa vyama vyingi.

"Kuna watu wanadhulumiwa kuanzia mchakato wa uteuzi ndani ya vyama, kwa maoni yangu mfumo wa mgombea binafsi, kama hapo awali, tangu kabla ya uhuru, urudishwe, kuwarudishia haki wagombea kupitia vyama, ambao wamedhulumiwa haki yao kupitia mchakato wa uteuzi ndani ya vyama.

"Ili kuepusha rushwa kwenye vyama turudi katika sheria kabla ya vyama vingi, Bunge likivunjwa hakuna anayezunguka majimboni. Awali ilikuwa ukibainika ulitoa rushwa, ubunge unavunjwa na kuzuiwa miaka 10," aliongeza Mlawa.

Pia alisema kuna baadhi ya sheria wakati wa mfumo wa chama kimoja zilikuwa nzuri, hivyo baadhi zirejewe ikiwamo Sheria ya Uchaguzi ambayo imeeleza mtu yeyote au mgombea ambaye hajaridhika na ushindi wa mgombea aende mahakamani.

"Vyama huwa vina mtindo wa kulinda Jimbo, kwa sababu hiyo wagombea hutumia rushwa, na akipita kwa mfumo huo kwa sababu chama kinalinda Jimbo, kitakaa kimya ili jimbo lisiende kwa mwingine.

"Kati ya masuala ambayo tulikutana nayo kama kamishna wa tume, wananchi walilalamikia sana rushwa kwenye uchaguzi. Hivyo kabla ya Uchaguzi Mkurugenzi wa Tume ya Uchaguzi (NEC), awape elimu wananchi, wawajue viongozi wenye kufuata kanuni, wawaambie uchaguzi utakuwa huru na haki," aliongeza.

**ADHABU YA KIFO**

Aidha, Mlawa ambaye pia aliwahi kuwa Wakili wa Serikali, alisema pia amezungumzia kuhusu adhabu ya kifo, akisema pamoja na kutotekelezeka, bado ina umuhimu wake na si muda wa kuifuta kwa kiwango cha nchi kama Tanzania.

"Wakati wa JK kulikuwa na mauaji yaliyokithiri ya watu wenye ualbino, waliuawa kwa Imani za kishirikina. Rais akasema sijawahi kusaini hukumu ya kifo kwa yeyote, ila kutokana na hili ikija kesi kuhusu mauaji hayo nitasaini mapema. Alipotangaza hivyo, mauaji yalikoma," alisema Mlawa.

"Wakati wa kufuta hukumu ya kifo kwa nchi kama Tanzania, haujafika, hususan kwa wahusika wa matukio ya mauaji yenye maslahi mapana kitaifa," alisisitiza.

# Bunge laagiza uchunguzi mkataba matrekta

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

SPIKA wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, ameiagiza Kamati ya Bunge ya Viwanda na Biashara kusikiliza na kuchunguza malalamiko na changamoto za mkataba wa ukopeshaji wa matrekta, kati ya wananchi wa mkoa wa Manyara na kampuni ya Ursus ya Poland.

Akitoa ufafanuzi jana kuhusu hoja iliyowasilishwa bungeni jijini hapa siku chache zilizopita na Mbunge wa Viti Maalum (Vijana), Asia Halamga, Dk. Tulia alisema amebaini kwamba kuna umuhimu wa kamati husika kushughulikia malalamiko ya wananchi ambayo yametolewa bungeni na wawakilishi wao.

"Hivyo nimeelekeza Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo, ikutane na Wizara ya Kilimo, Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, na Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC). Baada ya hapo, kamati isafiri kwenda mkoani Manyara ili kusikiliza changamoto za mkataba huu na athari zake hatimaye kupendekeza hatua za kushughulikia malalamiko hayo.

"Ili Bunge liweze kupata mrejesho kamili wa suala hili, nimeelekeza kuwa kamati husika baada ya kukamilisha kazi yake, iandae taarifa ambayo itawasilishwa bungeni wakati wa kipindi cha siku sita cha majumuisho ya bajeti kwa mujibu wa kanuni ya 124," alisema. Kwa mujibu wa Spika, kwa wakati huo anafikiri wabunge watapata suluhisho la changamoto hiyo ya matrekta ya Ursus, hivyo kwa bungeni watakuwa wameishauri serikali nini cha kufanya,

Kabla Spika hajatoa maelekezo hayo alisema: "Mtakumbuka hivi karibuni wakati wa mjadala wa makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka wa fedha 2023/24, ilibuka hoja kuhusu changamoto na athari zilizojitokeza katika mkataba wa ukopeshaji wa matrekta ya kampuni ya Ursus kufanyika kati ya Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC) na wakulima.

"Kwa kuwa mjadala huo ulivuta hisia kali miongoni mwa wabunge na wananchi walioathirika na mikataba hiyo nilagiza Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo, kukutana na Wabunge na wananchi wa maeneo hayo yaliyoathirika, ili kuwasikiliza na kubaini yanayolalamikiwa kuhusu suala hili."

Aprili 13, mwaka huu, Mbunge wa Viti Maalum (Vijana), Asia Halamga, tangu wananchi walipoingia mkataba na kampuni hiyo chini ya usimamizi wa NDC, hakuna vipuri vilivyoletwa nchini kwa mwaka wa pili sasa.

# Kazi 38 za ubunifu zaingia sokoni

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof.Adolf Mkenda, amesema kazi za ubunifu 38 zilizoibuliwa kwenye Mashindano ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu (MAKISATU), zimeanza kuingia sokoni ikiwamo ya mita ya maji ambayo kwa sasa inafanyiwa majaribio.

Pia amesema Wiki ya Ubunifu Tanzania imeanza kuchukua sura ya kimataifa na kwa mwaka huu kutakuwa na washiriki kutoka Afrika Kusini.

Akizungumza jana na waandishi wa habari jijini hapa kuhusu maadhimisho ya Wiki ya Ubunifu yatakayoambatana na maonyesho, itakayofanyika kuanzia Aprili 24 hadi 28 katika Uwanja wa Jamhuri Dodoma, Prof. Mkenda alisema tangu mwaka 2019, wizara kwa kushirikiana na wadau, imekuwa ikiendesha wiki hiyo na mashindano hayo ili kuimarisha mfumo wa ubunifu hapa nchini.

"Juhudi hizi zimetusaidia kuwa na mbalimbali za ubunifu ambazo tayari zimeanza kuingia sokoni. Kwa sasa ziko 38 ikiwamo ya mita ya maji inayofanyiwa majaribio ili ibiasharishwe,"alisema.

Alibainisha kuwa wiki hiyo kwa mwaka 2023 ni moja ya mikakati ya serikali ya kuongeza hamasa ya matumizi ya sayansi, teknolojia na ubunifu kama nyenzo ya kuharakisha maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

"Wiki ya ubunifu pamoja na mambo mengine, imekuwa ikiibua, kutambua na kuendeleza jitihada zinazofanywa na wabunifu na watumiaji wa bidhaa na inatoa fursa kwa wabunifu, wavumbuzi, watunga sera, wadau wa maendeleo na washirika wengine kukutana kujadili sera kanuni na miongozo mbalimbali kuhusu maendeleo ya sayansi, teknolojia na ubunifu,"alisema.

"Kwa mara ya kwanza safari hii tutakuwa na washiriki kutoka Afrika ya Kusini imeanza kuchukua sura ya kimataifa. Wiki itatanguliwa na maadhimisho ngazi za mikoa na halmashauri na yataratibiwa na kuendeshwa kwa ushirikiano na Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH), program ya Funguo chini ya UNDP, Ofisi ya Rais, Tamisemi na wadau wengine," aliongeza.

# Mchechu ataja vipaumbele uboreshaji mashirika

Na Mary Geofrey

MSAJILI wa Hazina, Nehemiah Mchechu, ametaja mambo manne yanayokwamisha ufanisi na utendaji wa mashirika na taasisi za umma ambayo ataanza kuyafanyia kazi.

Mchechu alisema hayo jana Jijini Dar es Salaam katika mkutano wake na wenyeviti wa bodi, watendaji na wakuu wa taasisi na mashirika ya umma na wakala za serikali. Kauli mbiu ya mkutano huo wa siku mbili ni 'Kuimarisha Usimamizi na Uendeshaji wa Taasisi na Mashirika ya Umma, Kuelekea Uwekezaji Wenye Tija kwa Taifa.'

Alisema tatizo kubwa ni kukosekana kwa maono ya muda mrefu kwa watendaji wanaoongoza taasisi na mashirika hayo, kutojua wanataka nini na nini kifanyike na wanakwenda wapi.

Kwa mujibu wa Mchechu, jambo la pili ni kukosekana kwa usimamizi thabiti hali ambayo inasababisha uzembe na ucheleweshaji wa kutotimiza wajibu kutokana kukosekana usimamizi.

Jambo la tatu, alisema ni aina ya uongozi uliopo kama una ufanisi au la na kwamba suala hilo wanalifanyia kazi katika uteuzi wa wakuu wa taasisi na kwamba wako baadhi wanaobainika kufanya kazi vizuri.

Alisema jambo lingine ni kuwa na mawasiliano kati ya viongozi wa bodi na watendaji wa taasisi hizo jambo ambalo wanalifanyia kazi kwa weledi.

"Na sisi tuna wajibu wa kusimamia na wajibu wa kuwa very clarity (wazi) ni wetu, nini tunakitaka kwenye taasisi ni wetu. Wajibu wa kuwawezesha kimitaji ni wetu na kubadilisha baadhi ya sheria zinazowafunga miguu wanashindwa hata kukimbia au kutimiza malengo yao ni wetu," alisema Mchechu.

Alifafanua kuwa kuna mambo wameyapokea na watayafanyia kazi na yale ambayo watendaji wa mashirika na taasisi wanatakiwa wafanye kazi yao ili matunda yaonekane.

"Huu ni mkutano wenye manufaa, wenye mafanikio ni mkutano wa kwanza na kila mwaka tutakapoanza kukutana, rasmi tutaanza Mei, jijini Arusha.

"Tukikutana tutakuwa tunaangalia nani kafanya vizuri nani kafanya vibaya, changamoto ni ipi tuitatue na mwisho wa siku tutakuwa na taasisi ambazo zina ufanisi kama zilizo kampuni kubwa za nje ambazo zinaingia hadi kwetu na zinakuwa zenye tija kwa serikali," alisema Mchechu.

Alisema mambo ambayo ofisi yake inafanyia kazi ni kupitia na kutengeneza mpango mkakati wa muda mrefu wa zaidi ya miaka 10 unaoakisi malengo makuu ya taasisi.

Mambo mengine, alisema ni kufanya marekebisho ya Sheria Ofisi ya Msajili wa Hazina Sura 370 kwa kuwa inakosa vifungu mahususi au kuwa na migongano na baadhi ya sheria za nchi, kuathiri utekelezaji wa majukumu yake kikamilifu na kwa tija.

"Leo (jana) nilikutana na kundi la watu 187 kutoka taasisi na mashirika ya umma yasiojiendesha kibiashara ambayo yanazijumuisha taasisi za vyuo, afya na maji. Katika mazungumzo yetu tulikuwa tunakumbushana wajibu, mipango iliyoko mbele yetu, wajibu ulioko kwenye taasisi hizo ili tuone kile wanachofanya na vile tunavyovihitaji.

"Kwa wale ambao hawategemezi faida ili sasa wapunguze utegemezi na ndio mchango wanaoweza kuutoa kwa serikali, wale ambao wanachangia waendelee kwa kuongeza ufanisi, kikubwa tunataka uwekezaji uliofanywa na serikali kwenye taasisi yoyote tuwe na ufuatiliaji wa karibu ili maslahi yake yaonekane," alisema Mchechu.

Mwenyekiti wa Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu (NBAA), Prof. Sylivia Temu, akizungumza kwa niaba ya washiriki wenzake, alisema mambo ambayo wanatakiwa kufanya baada ya mkutano huo ni kuangalia maslahi ya watumishi na kuandaa mpango wa kurithishana madaraka kwa sababu zinatakiwa kuwa endelevu.

# SKONGA ya EATV kupanda miti 1000 shule za Dar, Pwani



Waandaji wa kipindi cha SKONGA na wanafunzi wakiwa wanajiandaa kupanda miche ya miti.
**PICHA: MPIGAPICHA WETU**

Na Mwandishi Wetu

WAANDAAJI wa kipindi cha SKONGA kinachorushwa na kituo cha Televisheni cha EATV, wanatarajia kupanda miti 1000 katika shule za sekondari za mikoa ya Dar es Salaam na Pwani.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na waandaaji wa kipindi hicho, kazi hiyo ya upandaji miti itafanyika kwa udhamini wa kinywaji cha VIVO ENERGY.

Walisema kutakuwa na utoaji wa elimu kuhusu utunzaji mazingira pamoja na mada na maswali yatakayokuwa yanahusika kwenye vipindi.

Walisema katika kufanikisha mpango huo, utaratibu wa kazi hiyo ya upandaji miti utatolewa rasmi baadaye kwa wafanyakazi wote.

"Tunatarajia kutoa taarifa kwa wafanyakazi wote kuhusu mpango wa mradi huu, ili wapate taarifa sahihi.

"Kabla mradi kuanza rasmi, mitandao yetu ya kijamii pamoja na vipindi vyetu vya radio kuhusu mradi huo unaokuja," ilieleza taarifa hiyo.

Pia, walisema ufunguzi wa kazi hiyo kwa siku ya kwanza wahusika wakuu watakuwa ni waandaaji wa kipindi hicho cha SKONGA kwa asilimia kubwa katika kufanikisha.

"Taarifa itatolewa kwenye vyombo mbalimbali vya IPP ikiwamo vya habari vya EATV saa moja, ITV habari, na Mitandao ya kijamii ya EATV.Tutazungumza na wahusika wa kinywaji cha VIVO ENERGY na SKONGA KEVOO, Mwalimu, na Mwanafunzi ili kupata dhumuni rasmi la mradi huu kwa ajili ya habari na tutakuwa tunaweka taarifa ya kazi hiyo kwenye Mitandao yetu,"ilisema.

# Mikakati yaelekezwa bungeni mabadiliko sheria ya habari

Na Mwandishi Wetu

WADAU wa Haki ya Kupata Habari (CoRI) wamewaomba wabunge kuwasikiliza waandishi wa habari ili kubeba mapendekezo yaliyoachwa katika Muswada wa Mabadiliko ya Sheria ya Habari uliowasilishwa Februari 10 mwaka huu.

Akizungumza wakati wa mkutano wa CoRI jana jijini Dar es Salaam, Deodatus Balile, Mwenyekiti wa Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), alisema safari ya kuhakikisha tasnia ya habari inapata sheria chanya inaendelea.

"Tutakwenda kuzungumza na wabunge kuhusu athari zinazoweza kuifika tasnia ya habari kutokana na baadhi ya vifungu vilivyomo katika sheria na marekebisho yaliyofanywa na serikali ili watusaidie kurekebisha siku wakianza kujadili bungeni," alisema.

Balile alisema miongoni mwa vifungu ambavyo wanataka kirekebishwe na kuachwa kama kilivyo katika muswada huo, ni cha tisa ambacho kinampa mamlaka Mkurugenzi wa Habari (MAELEZO) kutoa leseni ya kuchapisha gazeti.

"Kwa mazingira yetu mtoa leseni ndiye mnyang'anyaji, hili tusingelipenda liendelee, hivyo tunakwenda kufanya uzengezi kwa wabunge ili wajue athari ya jambo hili kwa biashara," alisema.

Nevile Meena, Mjumbe wa Kamati ya Utendaji ya TEF, alishukuru serikali kutokana na dhamira yake ya kuifanya tasnia ya habari kuwa huru hasa kusimamia mchakato wa mabadiliko ya sheria ya tasnia hiyo.

Meena alisema kuwa licha ya kile kilichowasilishwa bungeni katika Muswada wa Mabadiliko ya Sheria ya Habari, kuwa na vipengele muhimu vya sheria hiyo vimeachwa nje.

"Kusudio jema la serikali tumeliona. Limefanya kile ilichofanya kwa lengo lilelile la kuboresha mazingira ya habari na waandishi wa habari, tunashukuru katika hilo maana baadhi tumeyaona kwenye muswada.

"Lakini sheria ikibaki kama ilivyopendekezwa katika muswada ule, hatuwezi kufanya kazi kwa uhuru na weledi tuliokusudia. Hatususi kwa kile kilichopelekwa, tutaendelea kushawishi kudai mabadiliko tena na tena. Mchakato wa sheria ni wa kuendelea, tukitoka sisi watakuja wengine kuendeleza tulipoishia," alisema Meena.

Deus Kibamba, Mjumbe wa CoRI, alisema ni heshima kuona serikali imeipa tasnia ya habari kuanzisha na kusimamia mchakato wa mabadiliko ya sheria ya habari mpaka hapa ulipo.

Alisema serikali ilikusudia kuondoa vikwazo na ndiyo maana Muswada wa Mabadiliko ya Sheria ya Habari una mambo mazuri ndani yake.

James Marenga, Makamu Mwenyekiti wa Misa-Tan ambaye pia ni wakili wa kujitegemea, alisema sheria ina upungufu ambao unapaswa upigiwe kelele na ufanyiwe marekebisho ili sekta ya habari ikue zaidi.

Alisema mapendekezo ya sheria yaliyotolewa na serikali, yamegusa maeneo tisa tu kati ya 21 yaliyopendekezwa yafanyiwe marekebisho.

Alisema miongoni mwa mapendekezo yaliyofanyiwa kazi na serikali na wanaunga mkono ni kifungu cha 5(1) kwa kumwondoa Mkurugenzi wa Habari (MAELEZO) kuwa mratibu wa matangazo kwa vyombo vya habari.

"Kifungu 38 kinachozungumzia kashfa ambavyo awali ilionekana ni jinai nacho kimefanyiwa marekebisho lakini mengi ni kupunguzwa kwa makosa na adhabu zake badala ya kuondoa," alifafanua.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Hatua ya kuifungia mitandao ni nzuri, kasi zaidi iongezwe

**SERIKALI** kupitia Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, mapema wiki hii ilitangaza kuwa imeifunga mitandao ya kijamii kadhaa kutokana na kukiuka maadili ikiwamo kuhamasisha ndoa za jinsia moja. Mitandao hiyo na idadi kwenye mabano ni tovuti (334), akaunti za facebook (361) akaunti za twitter (12), instagram (198) na vikoa 2,456.

Waziri mwenye dhamana na sekta hiyo, Nape Nnauye, alibainisha hayo bungeni alipokuwa akitoa majibu ya nyongeza katika swali lililoulizwa na mbunge akihoji ni hatua zipi ambazo serikali imezichukua dhidi ya watu wanaohamasisha mapenzi ya jinsia moja. Mbunge huyo alitaka pia kujua kama serikali iko tayari kupeleka bungeni Sheria ya makosa ya Kujamiiana ili kuifanyia marekebnisho na kuondoa upungufu uliomo.

Taarifa hiyo ya Waziri Nape ni habari njema kwa Watanzania hasa wale wanaopinga vitendo vya mapenzi ya jinsia moja ambavyo kwa sasa vimeanza kushamiri na hata kuwa tishio kwa maadili ya kitanzania.

Nchini Tanzania kuna sheria ambayo inakataza kinagaubaga mapenzi ya jinsia moja na kwa mujibu wa kifungu cha 154 cha Sheria ya Kanuni za Adhabu, Sura ya 16, kufanya mapenzi kinyume cha maumbile na mapenzi ya jinsia moja ni kosa la jinai. Sheria hiyo inakwenda mbali zaidi kwa kuweka wazi kwamba iwapo mtu atabainika kujihusisha na jambo hilo, adhabu yake ni kifungo cha maisha jela au kifungo kisichopungua miaka 30 jela.

Pamoja na kifungu hicho cha sheria, hivi sasa kumekuwa na ongezeko la vitendo vya ushoga na usagaji ambavyo vinachochea kuwapo kwa mapenzi ya jinsia moja. Mambo haya ni kinyume cha mila, desturi za kitanzania na Afrika kwa ujumla na kukithiri kwa vitendo hivyo ni kutokana na kuiga kwa utamaduni wa kigeni.

Baadhi ya nchi hasa Ulaya na Amerika zimeruhusu vitendo vya namna hiyo na kumekuwa na ndoa za jinsia moja tena zinafungishwa na viongozi wa dini lakini kwa Tanzania na Afrika kwa ujumla, ndoa hizi na vitendo vya kufanya mapenzi kinyume cha maumbile haviruhusiwi.


Lakini kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia ambayo yamehanikizwa na utandawazi, vitendo hivyo vimepenya mpaka katika ardhi ya Afrika, Tanzania ikiwamo na vijana wengi wameathirika na tabia hizo. Utandawazi si mbaya bali matokeo yake na matumizi ya teknolojia ni mazuri lakini si kuiga kila kitu kinachofanyika kwa wengine hata kama ni kibaya.

Tunatambua kwamba serikali imetoa uhuru wa vyombo vya habari na ule wa kutoa maoni lakini jamii ni lazima ifahamu kwamba hakuna uhuru wowote usio na mipaka. Kutokana na kuruhusu vyombo vya habari, mitandao mbalimbali ya kijamii imezidi kushamiri lakini mbaya zaidi baadhi inafanya mambo kinyume cha mila na desturi pamoja na kuvunja sheria za nchi kwa kuhamasisha vitendo viovu.

Kila uchao, baadhi ya mitandao inaibua mambo mengi yakiwamo yale ya kutisha au kuzua taharuki katika jamii. Baadhi ya mitandao imekuwa ikiwazushia viongozi mambo mbalimbali ikiwamo kudai aliyemuua mtu fulani ni huyu lakini ukifuatilia haina ukweli wowote.

Kama ilivyoelezwa awali, hatua iliyochukuliwa na serikali kuifunga mitandao hiyo ni nzuri na ya kupongezwa lakini jitihada zaidi zinahitajika ili kuibana na kuichukulia hatua mitandao yote inayokiuka sheria na maadili ya Kitanzania. Serikali kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) ichukue hatua kali dhidi ya mitandao hiyo na kama kuna upungufu katika sheria, yafanyike mabadiliko ili kuibana zaidi mitandao hiyo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Msawazo wa walimu mijini, vijijini ingepaswa utiliwe mkazo aina yake

**MOJAWAPO** ya vikwazo vikubwa kwenye elimu, ni baadhi ya shule hasa za vijijini kuwa na uhaba wa walimu, kitendo kinachosababisha wanafunzi kukosa baadhi ya vipindi, kwa kutokuwa na walimu wa masomo husika, ujumla wake kuporomoka kitaaluma.

Wakati shule za vijijini zinakumbwa na hali hiyo, za mjini walimu wamerundikana na huenda ndio wanaosababisha wanafunzi wa shule za vijijini kukosa baadhi ya masomo hasa ya sayansi.

Katika mazingira hayo, baadhi ya wazazi wanalazimika kufanya utaratibu wa kutafuta walimu wa kujitolea na kuwalipa posho kidogo, ili angalau watoto wao waweze kufundishwa masomo yote kuziba mapengo yaliyopo.

Wanatambua kuwa ubora wa elimu si majengo tu, bali ni pamoja na ufundishaji ambao unaenda sambamba na idadi ya kutosha ya walimu, ili kuhakikisha wanafunzi wote wanapata kile wanachokifuata shuleni.

Kwa hali hiyo, ni vyema serikali inapoajiri walimu, kipaumbele kiwe kwa shule za vijijini ambazo kiukweli zinakabiliwa na uhaba huo ambao kwa namna moja au nyingine unaweza kukwamisha maendeleo ya wanafunzi.

Kwa mfano, unaweza kukuta wanafunzi wanasoma masomo machache kwa sababu ya uhaba wa walimu, lakini kwenye mitihani ni lazima wafanye masomo yote, kitendo ambacho ni wazi hawawezi kufanya vizuri. Anatathminiwa kwenye mtihani kwa ambacho hajakisoma darasani, Hapo inaibua swali tena, maana ya mtihani ni nini?

Niseme iwapo shule zitakuwa na walimu wa kutosha, iko wazi wanafunzi watasoma masomo yote na kisha kuchagua wanayoyataka. Pia, wazazi na walezi watapunguziwa mzigo wa posho za kuwalipa walimu wa kujitolea.

Ikumbukwe kuwa, uhaba huo wa walimu umekuwa ukisababisha wazazi na walezi kubeba mzigo wa kuwalipia watoto wao masomo ya ziada 'twisheni' kwa wazazi wenye uwezo na kwa wale 'wenzangu na mimi...' Ninadhani kama walimu wangekuwa wa kutosha, kero nyingine zingepungua.

Hata hivyo, hivi karibuni serikali ilitoa maelekezo kwa Makatibu Tawala wa Mikoa yote Tanzania Bara, kufanya msawazo wa walimu kutoka shule zenye ziada na kuwapeleka katika shule zenye upungufu zaidi.

Naibu Waziri Ofisi ya Rais -TAMISEMI, David Silinde, alitoa maelekezo hayo bungeni Dodoma, wakati akijibu swali la mbunge aliyetaka kujua kuna mpango gani wa kutatuliwa changamoto ya uhaba wa walimu katika shule za pembezoni.

Katika ufafanuzi wake ni kwamba, tangu mwaka 2018/19 hadi mwaka 2021/22, serikali imeajiri jumla ya walimu 26,598 wakiwamo 16,640 wa shule za msingi na 9,958 wa shule za sekondari.

Kwa kuwa serikali inahakikisha walimu wanaajiriwa na kupangwa katika shule zenye uhitaji zaidi hususan zilizoko maeneo ya vijijini, basi hilo lingefaa lifanyiwe kazi haraka.

Ninaamini kila shule ikiwa ina walimu wa kutosha, hawatalazimika kufundisha vipindi vingi, huku wanafunzi nao wakikosa baadhi ya masomo kutokana na uhaba huo.

Msawazo wa walimu ambao serikali inaufanya ungegusa pia shule zenye walimu wengi na kuwahamishia vijijini badala ya kusubiri ajira na kuelekeza wengi huko, kwani suala la ajira linategemea bajeti.

Wakati serikali ikiboresha mfumo maalum wa maombi ya ajira na upangaji wa walimu uitwao Teachers Allocation Protocol (TAP), ambao shule zenye upungufu mkubwa wa walimu hususan zilizoko vijijini hubainishwa, ninadhani ipo haja ya kufuatilia shule za mijini ili kubaini wingi wa walimu waliopo.

# Watoto yatima wakumbukwa Sikukuu ya Eid

**Na Mwandishi Wetu**

KITUO cha watoto yatima 'Fadhillah Orphanage Centre' mkoani Pwani kimepewa msaada wa chakula kwa ajili ya Sikukuu ya Eid el Fitr na Kampuni ya Simu ya Halotel, kuonesha upendo na kuwaletea tabasamu watu wanaoishi katika hali ngumu, kupitia utekelezaji wa majukumu ya jamii ya watanzania.

Msaada waliopokea ni vyakula, mbuzi, na mahitaji mengine ya muhimu ya kijamii.

Wakikabidhi msaada huo, Mkuu wa Kitengo cha Masoko Halotel, Sakina Makabu, alisema msaada huo ni utaratibu wa kawaida wa kampuni hiyo kuikumbuka jamii hasa watoto waliopo katika mazingira magumu.


Sakina alisema, pia wamezielekeza ofisi zao mikoa mbalimbali Tanzania kusaidia makundi hayo kama walivyofanya Pwani.

Kituo cha Fadhila, kinalea na kusomesha watoto 168 ambao wote ni yatima kwa kuwapoteza wazazi wao. Watoto wengi kati yao walipitia changamoto nyingi, na kituo hicho kinatoa mazingira salama na ya upendo ambapo wanaweza kupata huduma na msaada wanaohitaji.

"Leo tunatoa mifuko ya kilo 150 ya mchele, kilo 50 za maharage, ndoo za lita 80 za mafuta ya kupikia, kilo 100 za unga wa mahindi, kilo 50 za sukari, Tambi mifuko 100, mbuzi wawili (2), sabuni za usafi wa mwili na za kufulia, pampas kwa mtoto asiyejiweza na Watoto wachanga, Pamoja na vifaa kwaajili ya shule. Zawadi hizi lengo lake kubwa ni kutoa tabasamu na upendo kwa watoto hawa katika sikukuu hizi za Eid Mubarak ili na wao waweze kusherehekea na kufurahia kama watu wengine," alisema Sakina

Mkurugenzi wa kituo, Sureya Shehe, alisema, "tunashukuru sana kwa mchango huu mkubwa kutoka Halotel. Utaleta tofauti kubwa kwa watoto hapa, ambao wanahitaji sana mahitaji ya msingi kama chakula na vifaa vya shule, na zaidi hasa kwa upendo huu kuwawezesha Watoto hawa kufurahia Sikukuu hii ya Eid Mubarak. Tunathamini jitihada hizi za Halotel kusaidia jamii yetu ya watanzania na tunatarajia waendelee kufanya hivi ili kuboresha maisha ya watanzania.

"Msaada wa Halotel kwa kituo hicho ni moja ya utaratibu ambao utaendelea kutekelezwa mara kwa mara ili kujenga mahusiano mazuri na jamii ambayo pia ni wateja na watanzania kwa ujumla. Utaratibu huo, unatekelezwa kufuatia sera bora ya kampuni hiyo kupitia program za kurudisha kwa jamii mbali na kutoa huduma bora za mawasiliano nchi nzima."



Mkuu wa Wilaya ya Ngara, Kanali Matias Kahabi (aliyevaa kofia) akiwa na Meneja Mkuu wa Mgodi wa Tembo Nickel, Manny Ramos (wa pili kulia), Meneja wa Afya na Usalama Mahala pa Kazi, Dk Kudra Said (kushoto) na Ofisa Mipango wa Wilaya ya Ngara, Labani Ildefonce, aliyemuwakilisha Mkurugenzi wa Halmashauri ya Ngara, Solomoni Kimilike, wakati Kampuni ya Tembo Nickel ilipokabidhi miradi ya uwajibikaji kwa jamii. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

# Ngara yanufaika na miradi ya mil. 200/- kutoka Tembo Nikel

**Na Mwandishi Wetu**

WILAYA ya Ngara imekabidhiwa miradi ya maendeleo ya jamii yenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 200 na Tembo Nickel.

Taarifa iliyotolewa na Kampuni hiyo ilisema miradi hiyo ni sehemu ya mchango wake katika uwajibikaji kwa jamii katika sekta ya elimu na afya kulingana na makubalino na Halmashauri ya Wilaya ya Ngara kupitia Mkataba wa Makubaliano (MoU) uliosainiwa Julai 7, 2022.

Mkuu wa Wilaya ya Ngara, Kanali Mathius Kahabi na viongozi wengine wa ngazi ya kijiji, walishuhudia makabidhiano hayo yaliyofanyika katika Shule ya Msingi Nyabihanga.

Kampuni hiyo imefanikiwa kukamilisha vyumba saba vya madarasa katika shule za msingi za Mukivumu, Gwenzanza, Muganza na Nyabihanga pamoja na madawati 20 kwa kila shule, madawati 80 pamoja na meza 80 kwa Shule ya Sekondari ya Rulenge

na kufanya jumla ya madawati 160 kwa shule tano, ukarabati vyumba vinne vya madarasa katika Shule ya Msingi Ruhuba na kukamilisha ofisi tatu katika Shule za Msingi Gwenzanza, Muganza na Nyabihanga.

Mchango huo katika sekta ya afya ni pamoja na kukamilika kwa ujenzi wa wodi ya wazazi katika zahanati ya Bugarama na msaada wa vifaa tiba katika zahanati

mbili za Bugarama na Rwinyana, sambamba na mafunzo kwa wahudumu wa afya ngazi ya jamii.


Jamii hodhi za Mradi wa Tembo Nickel ni washirika wa msingi katika uundaji wa thamani kwa pamoja kutoka kwenye Mradi wa Kabanga Nickel. Tunaamini katika ushirikiano kuanzia hatua za awali, endelevu na unaoshirikisha jamii zinazoguswa na mradi, mamlaka za wilaya na mkoa, wadau wa kitaifa na kimataifa ili kuhakikisha maendeleo endelevu. Kwa kuzingatia sheria za nchi na viwango vya kimataifa, "Tembo Nickel inaamini kuwa hii mbinu ina manufaa zaidi katika kuleta mahusiano ya kudumu na ni ya msingi katika kuwa mstari wa mbele kwenye uchimbaji na unufaikaji kupitia usawa katika manufaa ya kiuchumi," Meneja Mkuu wa Mgodi wa Tembo Nickel, Manny Ramos alisema.

Ushirikiano kati ya Tembo Nickel na serikali pamoja na Watanzania umeanzishwa rasmi kwa ajili ya kuchimba, kuchakata na kuchenjua madini ya nikeli ya kiwango cha kutengeneza betri na kuongeza thamani kwa pamoja kupitia usawa na uaminifu.

"Ingawa bado hatujaanza kuingiza faida kwa vile bado hatujaanza uzalishaji, bado tunaona umuhimu na wajibu wa kuchangia katika maendeleo ya jamii na nchi, hata katika hatua hizi ya awali. Tutaendelea kutekeleza miradi itakayokubaliwa kwa mwaka 2023. Ni dhamira ya kampuni kuhakikisha kuwa jamii inayozunguka mradi wetu inanufaika na uwepo wetu," alisema Rammos

Mkuu wa Wilaya ya Ngara, Kanali Mathias Kahabi, alisema: "Tembo Nickel ni mshirika wa kweli katika maendeleo, tayari tunafurahia matunda ya kuwa na mdau huyu mkubwa katika mkoa wetu, sio tu kupitia miradi hii ya maendeleo."

**KABWELA** **Na Fadhili Mohammed**



# Tangulia 'Mzee wa Mkono kwa Mkono', umefanya mengi, Musoma Vijijini, Butiama

**Na Sabato Kasika**

MUSOMA Vijijini mkoani Mara, wananchi walizoea kumwita kwa jina la 'Mzee wa Mkono kwa Mkono', kutokana na alivyojitoa kwa hali na mali kuchangia maendeleo ya jimbo hilo.

Nimrod Mkono alikuwa mwanasiasa ambaye jina lake lilianza kuvuma katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2000 ambao aliibuka na ushindi wa kishindo kupitia CCM.

Akiwa Mbunge wa jimbo hilo kwa mihula mitatu kuanzia mwaka 2000 hadi 2005, Mkono alijipatia umaarufu mkubwa kutokana na alivyokuwa karibu na wapigakura wake katika shida na raha.

Kaulimbiu yake ya Mkono kwa Mkono anapofika katika misiba au sherehe na kuchangia chakula au fedha, ilimpa umaarufu mkubwa ambapo likitoka jambo lolote alishirikishwa.

Mkono na kaulimbiu yake hakuishia hapo, bali pia katika shughuli za maendeleo kuanzia kwenye elimu, afya na kwingineko, alisaidia ujenzi wa sekondari na zahanati jimboni humo kwa kutoa vifaa au fedha.

Aliweza kuzungukia jimbo zima kirahisi kwa kutumia usafiri wa helkopta, alipoonekana angani tu utasikia wananchi wanasema; 'Mzee wa Mkono kwa Mkono huyo anatembelea jimbo'.

Kupitia usafiri huo, ilikuwa ni rahisi kwa Mkono kuonana na wananchi mara kwa mara, kuzungumza nao, kujua kero zao na kutatua zile ambazo zilizokuwa kwenye uwezo wake.

Mwaka 2015, Jimbo la Musoma Vijijini liligawanywa na kupatikana la Butiama ambalo amelitumikia hadi mwaka 2018 alipokwenda nchini Marekani kwa matibabu, bahati mbaya amefariki dunia.

Lakini kutokana na kujitoa kwake kwa ajili ya Jimbo la Musoma Vijijini, alichukuliwa kama mwana maendeleo, kwa kuwa alijenga shule nyingi baadhi zikiwa ni Chifu Ihunyo iliyopo kijijini kwao Busegwe.

Nyingine ni Shule ya Msingi Busegwe, Chifu Wanzagi, Chifu Oswald Mang'ombe, ambayo sasa Chuo cha Kilimo cha Mwalimu Nyerere, Shule ya Sekondari Butuguri, pia akafufua Shule ya Sekondari Kasoma.

Ushiriki wa mwanasiasa huyo uligusa hata kwenye chama chake, kwani ameshiriki kuanzia ngazi ya matawi kwa kujenga ofisi za CCM katika maeneo mbalimbali ya Musoma Vijijini na Butiama kwa nyakati tofauti.

Mwanasiasa huyo ndiye aliyehusika kwa kiasi kikubwa kwenye ujenzi wa ofisi ya CCM ya Mkoa wa Mara, lakini kwenye harambee ya kuchangia chama mkoani humo, katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2005.



Marehemu Nimrod Mkono

Mwanzoni mwaka 2018, nilizungumza naye kwa njia ya simu na kumuulizia ratiba ya kwenda jimboni kwake Butiama, akasema kwa kifupi tu kwamba, hakuwa na ratiba hiyo.

Baada ya hapo, taarifa ambazo hazikuwa rasmi zikawa zinaeleza kuwa mbunge huyo wa zamani wa majimbo ya Musoma Vijijini na Butiama yuko Marekani ingawa haikufahamika anafanya shughuli gani.

Hata hivyo, juzi familia kupitia kwa mdogo wake, Zadock Mkono ikaeleza kuwa amefariki dunia akiwa katika matibabu nchini humo ambapo sasa mipango ya kurudisha mwili nyumbani inaendelea.

Tangulia mzee wa 'Mkono kwa Mkono', umefanya mengi Musoma Vijijini na Butiama ukiwa Mbunge wa majimbo hayo kwa nyakati tofauti. Ninaamini wananchi watakukumbuka kwa mengi.

Maendeleo kwenye sekta ya elimu ambayo Mkono alianzisha tangu alipokuwa Mbunge yamerahisha Musoma Vijijini kuwa na sekondari kwa kata zote 21 ambazo baadhi sasa zina sekondari mbili.

Pale ambapo Mbunge huyo aliishia na kwenda Butiama, pameendelezwa na mbunge wa sasa Profesa Sospeter Muhongo hadi kuzifanya baadhi ya kata kuwa na sekondari zaidi ya moja.

Kwenye afya nako jitihada za kujenga zahanati kila kijiji na kituo cha afya kila kata zinaendelea, katika majimbo yote mawili ya Musoma Vijijini na Butiama ambayo aliwahi kuyaongoza.

Mkono aliyezaliwa Agosti 18, 1948, ameacha mjane Mary. Pia atakuwa ameacha alama katika majimbo hayo kwa kuchangia shughuli za maendeleo akitumia kaulimbiu yake ya 'Mkono kwa Mkono'.

## AMF, TUHEDA wasaidia wenye mahitaji

**Na Maulid Mmbaga**

TAASISI ya Asma Mwinyi Foundation (AMF) ikishirikiana na Shirika la Tanzania UK Healthcare Diaspora Association (TUHEDA), wametoa msaada wa vyakula katika kituo cha kulea watoto wenye mahitaji maalum cha Malaika ikiwa ni mwendelezo wa utoaji sadaka ya futari wakati huu wa ibada ya mfungo wa mwezi Mtukufu wa Ramadhani.

Akizungumza jana baada ya kukabidhi msaada huo kwa kituo hicho kilichopo Wilaya ya Mkuranga, mkoani Pwani, mwakilishi wa AMF wilayani hapo, Hassan Kambangwa, alisema vitu vilivyotolewa ni unga, maharage, mchele na mafuta ya kupikia, huku ikielezwa kuwa uhaba wa chakula ni moja ya changamoto zinazowakabili watoto katika kituo hicho.

Alibainisha kuwa taasisi hiyo ambayo lengo lake kuu ni kusaidia makundi maalumu ikiwamo wanawake na watoto, pia imekuwa ikitoa misaada katika nyanja tofauti zikiwamo hospitali, nyumba za ibada, vituo vya kulea watoto wenye mahitaji maalum na uchimbaji wa visima vya majisafi kwa ajili ya jamii.

Mlezi wa watoto katika kituo hicho cha Malaika Emanuel Tomas, alibainisha kuwa katika kituo hicho wanalea watoto zaidi ya 80 na sio mara ya kwanza AMF kufika na kusaidia mahitaji tofauti ya watoto hao, chakula walichopatiwa kitawasaidia kwa kiasi kikubwa.

"Kituo chetu kinachangamoto nyingi, ikiwamo ya chakula, ada ya kuwasomesha watoto, mashuka na neti, pia niwaombe wafadhili wengine waguswe na watoto hawa, watu pekee ambao tunaweza kuwalea watoto hawa ni watanzania wenyewe na tunaishukuru sana taasisi ya Asma Mwinyi kwa jitihada inazoendelea kuzionyesha kwa kuwasaidia watoto hawa," alisema Tomas.

Mmoja wa watoto wanaolelewa katika kituo hicho, Salumu Omari, aliishukuru AMF kwa kuwasaidia chakula na kutoa wito kwa wadau wengine kuwakumbuka.

## Muswada kubadili fidia wanaoshambuliwa na wanyamapori wanukia

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imesema inatarajia kupeleka bungeni muswada wa marekebisho ya Sheria ya Kifuta Machozi na Jasho ya Mwaka 2011 ili kuboresha viwango vya fidia kwa waathirika wa wanyamapori wakali na waharibifu.

Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mary Masanja alitoa ahadi hiyo bungeni jana alipojibu swali la nyongeza la Mbunge wa Nanyumbu (CCM), Ally Mhata.

Katika swali lake, mbunge huyo alitaka kujua kama waziri yuko tayari kuwasilisha muswada bungeni kurekebisha viwango ili wananchi walipwe haki kulingana na hali halisi.

"Fidia wanazolipwa waathirika ni ndogo kuliko hali halisi ilivyo, waathirika hawa wanaopoteza maisha, fidia ni ndogo, wanaopata ulemavu fidia ni ndogo na wanaoharibiwa mashamba yao pia fidia ni ndogo, Je, waziri yupo tayari kuleta muswada huo bungeni?" alihoji.

Akijibu swali hilo, naibu huyo alisema sheria hiyo ya mwaka 2011 iliyopitisha kifuta machozi na kifuta jasho ilikuwa na lengo la kumfuta machozi mwathirika, lakini ukiangalia namna ya kufidia maisha ya mwananchi au ulemavu ni ngumu kufidia.

"Fidia hii ilikuwa kwa madhumuni ya kumshika mkono ili kuona kuwa serikali ipo pamoja naye, mwaka jana katika Bunge hili tulipewa maelekezo ya kupitia upya kanuni yake inayohusiana na kufuta machozi na jasho na hivi karibuni italetwa katika Bunge hili ili kuipitia na tuweze kuongeza kiwango hiki na kanuni zirekebishwe," alisema.

Katika swali la msingi, Mbunge Mhata alitaka kujua idadi ya wananchi wa Jimbo la Nanyumbu waliofidiwa kutokana na uharibifu uliofanywa na tembo katika mashamba yao.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri huyo alisema kwa mwaka 2022/23, wizara ilipokea maombi manane kutoka kwa wananchi wa vijiji vya Michenjeuka, Lukula, Masuguru, Murumba na Mpombe walioathiriwa na matukio ya wanyamapori wakali na waharibifu katika Halmashauri ya Nanyumbu.

Alisema, baada ya taratibu za malipo kukamilika mnamo Machi 21, mwaka huu, wizara ilifanya malipo ya kifuta jasho ya Sh. milioni 5.1 kwa wananchi saba wa vijiji vya Michenjeuka, Lukula, Masuguru na Mpombe walioharibiwa mazao.

**POPO DAR**

Katika hatua nyingine, Naibu Spika wa Bunge, Mussa Zungu alitaka serikali kutoa kauli kuhusu kukithiri kwa popo katika Kata ya Kivukoni.


"Kata ya Kivukoni katika Jimbo la Ilala kuna kero ya popo waharibifu, wanachafua mazingira, wananchi wameshalalamika mpaka leo bado wapo, hebu tueleze mnatoa kauli gani ya kuondoa popo hao katika Kata ya Kivukoni?" alihoji kiongozi huyo wa Bunge ambaye pia ni Mbunge wa Ilala.

Naibu Waziri Masanja alikiri kuwapo tatizo hilo kwenye maeneo ya Kivukoni jijini Dar es Salaam hususan maeneo yanazozunguka Ikulu.

Alisema, serikali imeshaanza kuyafanyia kazi na walishawahi kupuliza dawa kuwapunguza lakini changamoto wanayoipata ni kwamba wana tabia ya kurudi baada ya muda fulani.

"Sasa tumeshaanza utaratibu kwa kushirikiana na taasisi ya Utafiti ya Wanyamapori Tanzania (TAWIRI) kutafuta mbinu mbadala na kuhakikisha tunawaondoa kabisa, nikuahidi kabla ya Bunge hili la bajeti kumalizika tutakuwa tayari tumeshakamilisha utaratibu wa kuwaondoa," aliongeza.





Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro, mkoani Manyara, Dk. Suleiman Serera (katikati), akizungumza na viongozi mbalimbali wa kata ya Loiborsiret, akiwemo Diwani wao Ezekiel Lesenga Maridadi (watatu kushoto), alipotembelea kukagua ujenzi wa Kituo cha Afya Loiborsiret juzi. **PICHA: GIFT THADEY.**

# Vijana wabunifu watakiwa kutatua matatizo yanayowasibu wananchi

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

MKUU wa Wilaya ya Arumeru, Emmanuela Kaganda, amewaagiza vijana wanaojishughulisha na masuala ya ubunifu kuangalia matatizo yanayowakabili wananchi na kuyachukulia kama fursa kwa kubuni vitu ambavyo vitasaidia kutatua matatizo hayo.

Alitoa agizo hilo jana wakati akizindua wiki ya ubunifu kwa mwaka 2023 mkoani Arusha, iliyoandaliwa na kituo cha ujasiriamali na ubunifu cha WSHA, kwamba zaidi ya vijana wabunifu 100 walishiriki katika uzinduzi huo. Alisema jamii imekuwa ikikabiliwa na matatizo mbalimbali ambayo yanahitaji kupatiwa ufumbuzi wa haraka, kwamba kupitia ubunifu ndiyo njia pekee ya kuja na majibu ya matatizo hayo.

"Nawaagiza wabunifu wote tumieni matatizo yaliyoko kwenye jamii kama fursa ya kubuni vitu mbalimbali ambavyo vitaweza kuwatoa sehemu moja kwenda nyingine na kujikwamua kiuchumi.

Mkurugenzi wa Kituo cha WSHA, Isaack Shayo, alisema wiki ya ubunifu inafanyika nchi nzima na kila mkoa wanaadhimisha wiki hiyo na mada kuu kwa mwaka huu ni 'Ubunifu kwa uchumi shindani'.

Shayo alisema wiki hiyo ni muhimu kwa wabunifu kwa kuwa wanapata fursa ya kukutana na wadau na kujifunza masuala ya ubunifu na kuona vitu vipya na kupata uzoefu zaidi.

Naye Mkurugenzi wa Kampuni ya Msichana Imara, Eliwilimina Buberwa, alisema endapo vijana wataamua kujikita zaidi katika masuala ya ubunifu itawasaidia kuondokana na tatizo la ukosefu wa ajira na wataweza kujiajiri.

# TCRA yawataka wasafirishaji vipeto, vifurushi kujisajili

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

MAMLAKA ya Mawasiliano nchini (TCRA), imewaelekeza wasafirishaji wa vipeto na vifurushi ndani na nje ya nchi kuhakikisha wanajisajili ili huduma hiyo ifanyike kwa usalama zaidi.

Akizungumza jana jijini Arusha katika kikao cha wasafirishaji wa vipeto na vifurushi, Ofisa Mwandamizi Mkuu TCRA), Abel John, alisema ni vizuri kila mtu anayefanya huduma hiyo aifanye kwa mujibu wa sheria na taratibu za nchi. b"Wasafirishaji wanapojisajili na kujulikana inamhakikishia mteja kuwa na uhakika na usalama wa mzigo wake anaosafirisha na pale unapokwama mahali inakua rahisi kwa TCRA kufuatilia na kujua tatizo liliko,"alisema.

Ofisa huyo alisema kila biashara ni vizuri ikafanyike kwa kufuata utaratibu ili iwe rahisi kwa wasimamizi wa mamlaka kuratibu .

"Zisiposajiliwa inakua ngumu kuratibu au kufuatilia huduma hizo kwetu, mfano kwa sasa biashara za huduma mbalimbali mtandaoni ni kubwa kama hatutakua na utaratibu wa kuratibu hatutafahamu vitu vinavyoingia,"alisema.

Ofisa Mwanadamizi Mkuu Kitengo cha Mawasiliano TCRA, Semu Mwakanjala, alisema hadi sasa sekta ya usafirishaji vifurushi na vipeto imepiga hatua kubwa.

Alisema huduma hizo ni muhimu kwa kuwa zinaendelea kutumika na kupanuka na kuna umuhimu kwa watoa huduma kuhakikisha wanazitoa kwa mujibu wa sheria zilizopo.

Vilevile aliwaomba wanaotoa huduma hizo endapo leseni zao za biashara zimefikia ukomo wazihuishe ili waendelee kutoa huduma hizo bila wasiwasi.

Posta Masta Mkuu wa Mkoa wa Manyara na Arusha, Athuman Msilikale, aliwasihi wasafirishaji wasikate tamaa kwa kuwa huduma hiyo bado inatumika na hasa barua za kibiashara kati ya taasisi na taasisi tofauti na zile za kirafiki ambazo zimepungua kwa sasa sababu ya kukua kwa teknolojia ya mtandao.

# Waandishi wa habari wanolewa utambuzi vyanzo vya habari feki

**Na Shaban Njia, Aliyekuwa**
ARUSHA

WAANDISHI wa habari zaidi 30 wamepatiwa mafunzo ya kutambua habari za uongo zinazochapishwa kwenye mitandao na kuzua hataruki katika jamii.

Mafunzo hayo yalitolewa kwa muda wa siku mbili na shirika la Africa Check kwa kushirikiana na Nukta Africa yaliyofanyika mkoani Arusha.

Mtoa mafunzo hayo, Alphonce Shiundu kutoka Africa Check, alisema lengo la kuandaa mafunzo hayo ni kuwaelimisha waandishi wa habari kuzitambua habari, picha, habari za sauti na video zenye ukweli zinazochapishwa mitandaoni bila kupotosha jamii.

Alisema habari yenye ongo inayochafua viongozi mbalimbali wa nchi au watu maarufu inasambaa zaidi ukilinganisha na habari ya ukweli.

Alisema kuna umuhimu kabla ya kuchapicha habari yoyote kila mwandishi anatakiwa kuwa makini na kuhakiki kabla ya kuchapisha ili kuepuka kupotosha huo. "Ndugu zangu habari ya uongo inasambaa haraka sana tofauti na za ukweli, zinachafua viongozi wetu wa nchi, wanasiasa hasa kipindi cha uchaguzi na watu maarufu, kabla ya kuchapisha hasa zile zinazorushwa katika mitandao yetu ya kijamii tuhakikishe tunahakiki ukweli wake ili kuepuka kupotosha wananchi," alisema Shiundu.

Mtafiti Mwandamizi, Makinia Juma, alisema baadhi ya vyombo vya habari hasa vya mtandaoni vimekuwa vikitengeneza habari nyingi za uongo kwa ajili ya kutafuta wasomaji katika kurasa zao jambo ambalo ni ukiukwaji wa maadili. Hivyo, alivitaka vyombo vya habari kuhakikisha kabla ya kuchapisha habari kufuatilia, kutambua ukweli wake na kuacha kukimbilia kuchapisha kwa kile ambacho hawana uhakika nacho hasa walichokiona katika mitandao ya kijamii.

Pia aliwataka waandishi wa habari kuhakikisha mafunzo hayo yanawafikia na waandishi wengine waliokosa nafasi ya kushiriki kwa kuelekeza hatua za utambuzi wa kutambua habari za uongo.

Mmoja wa washiriki wa mafunzi hayo kutoka Redio ya CFM ya jijini Dodoma, Ferista Richard, alisema alikuwa anashindwa kutofautisha habari ya uongo na ile ya kweli hasa zile za sauti na video.

Alisema kila kilichokuwa kinachapishwa katika mitandao ya kijamii alikiamini kwa sababu wale wanaopotosha umma walikuwa wakichukuliwa hatua na serikali kupitia Mamlaka ya Mawasiliano (TCRA).





## Wafanyabiashara Soko la Maswa walia ubovu wa vyoo

**Na Alex Sayi,** MASWA

WAFANYABIASHARA wa Soko kuu la Maswa Mkoani Simiyu wameuomba uongozi wa Halmashauri ya Wilaya kuboresha huduma ya choo ili viendane na ubora wa soko hilo kwa lengo la kudhibiti magonjwa ya milipuko.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti wafanyabiashara hao walidai kukabiliana na adha katika huduma ya choo kilichopo kushindwa kukishi mahitaji yao pamoja na hali ya ubora wake kuwa chini na kuhatarisha afya zao pamoja na wateja wao.

Mmoja wa wafanyabiashara katika soko hilo, Rahel Chuwa alisema: "Licha ya hali ya maisha kupanda bado halmashauri imepandisha ushuru wa meza kwetu kutoka Sh.20,000 hadi Sh.30,000 kwa mwaka na bado hata miundombinu haiboreshwi, tunaomba waboreshe pia miundombinu kwani tayari tunalipia ushuru tena kwa wakati".

Naye Mwenyekiti wa soko hilo, Naftali Joramu alisema kuwa kwa sasa halmashauri inaendelea na ukarabati wa miundombinu sokoni hapo na tayari Sh.milioni 42 zimetumika kujenga vizimba vipya na Sh.milioni 55 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa vibanda vipya vya kisasa na vyenye ubora.

Akieleza juhudi za utatuzi wa adha hiyo, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya Maswa, Simon Berege alisema kuwa halmashauri kwa mwaka wa fedha 2022/2023 imetenga Sh.mil 200 kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa vibanda vya ghorofa sokoni hapo pamoja na kuboresha huduma nyingine za muhimu.

Alisema: "Tayari tumemwelekeza mhandisi kuweka suala hilo katika mchoro ili wakati watekelezaji mwingine nalo linashughulikiwa lengo ni kulifanya soko hili liwe la kisasa".

# Jiwe la maajabu lazua hofu wakazi Nyamagana

**Na Vitus Audax,** MWANZA

WAKAZI wa Mtaa wa Mkapa Kata ya Igoma wilayani Nyamagana mkoani Mwanza, wameiomba serikali kupeleka wataalamu wa miamba katika mtaa wao ili kupasua jiwe ambalo limezua hofu baada ya kuonekana likisogea katika makazi yao.

Jiwe hili linajongea baada ya kunyesha kwa mvua kubwa huku likidondosha udongo uliokuwa umelishikilia.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti wananchi hao walisema jiwe hilo kubwa limekuwa likisogea kwenye makazi yao, kwamba limekuwa tishio kwao na watoto.

Mmoja wa wakazi hao kutoka Mtaa wa Mkapa, Farida Ramadhan alisema: "Kwanza udongo uliokuwa umelishikilia ulishushwa na mvua ambazo zimekuwa zikinyesha mara kadhaa huku jiwe lililokuwa limelishikilia nalo likaanza kupasuka, hivyo kutokana na sisi kuwa katika mteremko tunahofu jiwe hili likiachia lazima lifikie kwenye nyumba yetu na kuleta madhara".

Mkazi mwingine wa Mtaa wa Mkapa, Philimon Ludovick, alisema njia pekee ya kulizui jiwe hilo ni kupelekwa wataalam wa miamba ili waweze kujua namna ya kuliondoa pasipo kuleta madhara, kwamba endapo likipasuliwa kawaida linaweza kuporomoka katika nyumba jirani na kusababisha hasara.

Akizungumza na Nipashe Mwenyekiti wa Mtaa waMkapa, Fadhil Emmanuel alisema wamefanya juhudi mbalimbali ikiwa ni pamoja na kulishirikisha Jeshi la Polisi ambalo liliwashauri kuchangia fedha na kuwalipa watu wanaopasua miamba ili walipasue.

Kaimu Kamanda wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Kamila Laban, alifika katika eneo hilo na kuwataka wananchi mkoani humo kufuata sheria za ujenzi husani katika maeneo ya milimani.

Alisema: "Tumeliona jiwe hili kweli ni hatarishi na muda wowote linaweza kuporomoka na kuangukia nyumba zaidi ya saba kutokana na kuwa mlimani lakini tutaleta wataalamu wa miamba kutoka maeneo mbalimbali ikiwa ni pamoja na wale wa migodini ili wasaidie kulipasua kabla halijaleta madhara".



Mwanasheria kutoka Chama cha Wanasheria Watetezi wa Mazingira kwa Vitendo (LEAT), Clay Mwaifani akitoa elimu ya msaada wa kisheria kwa wananchi wa Mpomvu, kata ya Mtakuja, Halmashauri ya Geita Mji mapema wiki hii, kwa lengo la kuwasaidia kutatua matatizo yao ya migogoro mbalimbali kwa mujibu wa sheria na siyo kujichukulia sheria mkononi. **PICHA: MARCO MADUHU.**

# Watu 21 mbaroni tuhuma kuiba miundombinu ya maji

**Na Mohab Dominick,** TABORA

JESHI la Polisi mkoani Tabora limewakamata watu 21 kwa tuhuma za wizi wa vifaa vya miundombinu ya maji kutoka Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Tabora Mjini (TUWASA). Watu hao walikamatwa baada ya kuundwa kwa kikosi kazi kilichojumuisha askari polisi, watumishi TUWASA, halmashauri na vyombo vingine kwenye operesheni zinazoendelea katika Wilaya ya Tabora.

Akizungumza na waandishi wa habari, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tabora Kamishna Msaidizi wa Polisi, Richard Abwao, alisema katika operesheni hiyo, askari wake walifanikiwa kukamata vitu mbalimbali vilivyoibiwa.

Katika tukio lingine, Kamanda Abwao alisema Aprili 15 mwaka huu katika Kitongoji cha Utusini Kijiji na Kata ya Misha Wilaya na Mkoa wa Tabora, Benedictor Shaban Modest (40) alikutwa amefariki dunia kisha kufukiwa kwenye shimo, huku chanzo kikiwa ni wivu wa mapenzi.


Kamanda Abwao alisema mtu huyo alipigwa na kitu kizito kichwani kisha kumfukia katika shimo ambalo lilichimbwa na mtuhumiwa huyo ambaye kamanda hakumtaja jina kwa sababu za kiupelelezi.

Kamanda Abwao alidai kuwa mwili wa marehemu umehifadhiwa katika Hospitali ya Rufaa Mkoa wa Tabora kwa ajili ya uchunguzi na mtuhumiwa anashikiliwa na baadaye atafikishwa mahakamani baada ya upelelezi kukamilika.



Ukurasa 12

‘Kuchumbia mazao’ na ujazo wa lumbesa unavyodhulumu jasho la mkulima shamba




Ukurasa 13

Maradhi ya bodaboda, daladala yanapoambukiza askari trafiki

# BUFE

IJUMAA APRILI 21, 2023
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA



Ukurasa 14

## Kahitimu sheria akaweka cheti pembeni, kazama kwenye ujasiriamali ‘njia nyeupe’

UCHUMI

# Mkataba alioshuhudia Samia, kupaisha uchumi mtaji wa madini Sh. trilioni 1.6

- Neema ndani ya Songwe, Lindi, Ulanga...
- Lengo lake sekta itoe 10% GDP lakaribia

**Na Mwandishi Wetu**

HADI sasa Tanzania ni nchi inayomiliki rasilimali nyingi zikiwamo madini ambayo yana uwezo mkubwa kukuza uchumi wake. Pia, hilo linaendana na uhalisia, kiongozi mkuu wa nchi, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, naye yuko ndani ya mstari huo akionyesha shauku ya kupeleka mbele gurudumu la maendeleo ya Watanzania, ikiwamo kutumia maslahi yao.

Hiyo inaendana na kuwapo rasilimali za kimsingi kitaifa zenye nafasi ya kuhamasisha mwamko wa uchumi kitaifa, kama vile ardhi safi na yenye rutuba, milima, bahari, mbuga za wanyama, zilizozagaa kila pembe ya nchi.

Tanzania hadi sasa imebahatika kuwa na ardhi kubwa na rasilimali zinazochochea uchumi wa nchi. Hapo ndani yake inajumuisha madini yanayotafutwa duniani, kwa ajili ya uzalishaji bidhaa mbalimbali.

Ikirejewa miaka miwili na ushee iliyopita wakati Rais Dk. Samia anapewa mikoba ya mtamgulizi wake, marehemu Rais, Dk. John Magufuli, aliamua kukuza na kuendeleza miradi ya kimkakati aliyokabidhiwa kuiendeleza, akiwa na shauku kuona nchi inapiga hatua kubwa za kiuchumi kwa kuboresha sekta ya madini.

Hadi sasa Tanzania imo katika maeneo yaliyobarikiwa kuwa na madini adimu kama vile dhahabu, tanzanite, chuma, nicol, shaba, ruby, almasi, chokaa, chumvi, gesi, uranium na makaa ya mawe, yakipatikana kwenye mikoa iliyobahatika kama vile; Lindi, Morogoro, Mara, Shinyanga, Tabora, na Songwe yakiwa




Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akishuhudia Waziri wa Madini, Doto Biteko na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Jaji Eliezer Feleshi, wakitia saini Mkataba wa Makubaliano ya Msingi kati ya serikali na kampuni ya uchimbaji madini Peak Rare Earth, ya Australia iliyowakilishwa na Mwenyekiti Mtendaji wake, Russell Scrimshaw wa pili (kulia) na Ofisa Mtendaji Mkuu wa kampuni hiyo, Bardin Davis, Ikulu Chamwino Mkoani Dodoma, Aprili 17 mwaka huu. **PICHA: MTANDAO**

na maeneo nyeti ya madini.

Ni siku chache tu zimepita, Rais Dk. Samia amezungumza namna nchi inatarajiwa kwenda mbele ikisimamia sekta ya madini inayoongozwa na Waziri wake, Dotto Biteko, aliyepewa jukumu hilo tangu zama za mtangulizi, hayati Dk. Magufuli. Ni uwasilisho wake, wakati Rais anashuhudia utiaji saini mikataba ya uchimbaji madini ya kinywe kwa mikoa ya Lindi, Morogoro na Songwe.

Inaelezwa kuwa jambo la kuchochea mwamko wa uchumi nchini, hasa ikizingatiwa mikataba inayoangukia uwekezaji mkubwa inaletwa nchini na ina faida kubwa kutoka kwenye mauzo. Pia, hisa za serikali ndani ya uwekezaji wa miradi hiyo inapaa, jambo ambalo matokeo yake yanaangukia tafsiri ya kiuchumi, uwekezaji hisa nchini na uchumi kitaifa, unakuwa katika thamani ya juu; vyote vikiangaliwa vinabaki kuchangia kasi ya ukuaji uchumi kitaifa.

“Mikataba mipya iliyosainiwa na serikali italeta nchini mtaji wa Dola Milioni 667 (takriban Shilingi za Kitanzania Trilioni 1.6) katika kipindi hiki kigumu cha kiuchumi duniani na kuleta ahueni kwa nchi yetu. Mikataba yote hii ya madini ya kimkakati kupitia sisi na wenzetu kampuni tatu za nchini Australia, ni sehemu ya kuipaisha Tanzania katika ramani ya dunia, kwa kuangalia eneo lote la uchimbaji, uchakataji na usafirishaji kwenye mataifa makubwa yaliyoweka mkazo kwenye sekta hiyo kupitia nchi yetu,” anasema Rais Dk. Samia.

Hadi sasa, zama za uongozi wa nchi unaoendelea Awamu ya Sita, mchango wa sekta madini kwenye pato la taifa umeongezeka kwa kiwango kikubwa. Hadi Desemba mwaka jana, inatajwa ilikuwa asilimia 9.7, ikikaribia lengo la Rais Dk. Samia asilimia 10 ya Pato la Taifa au zaidi, ifikapo mwaka 2025.

Ishara za kiuchumi zinaonyesha sekta hiyo kufanikiwa sana, kuvuka malengo yake. Pia, ni mkakati usio mbali na kuwalinda, pia kuwainua wachimbaji wadogo, ikibeba tafsiri ya kumwinua Mtanzania mmoja mmoja.

“Mchango kwa wachimbaji wadogo kwenye sekta hii umeongezeka maradufu, kufikia asilimia 40 chini ya uongozi wa Rais Samia, kutoka asilimia 20 aliyoikuta alipoingia madarakani” anasema Waziri Biteko na kuongeza: “Serikali itaendelea kuongeza uwezeshaji, ikiwamo kuongeza kasi katika michakato mbalimbali katika maeneo ya wachimbaji wadogo, ili watumie vifaa na nyenzo za kisasa kama njia ya kuongeza ufanisi kwenye sekta hii muhimu kwa nchi yetu.”

Rais Dk. Samia anasema, uwekezaji huo tajwa, unaenda kwenye mikoa ambayo bado uchumi wake haujatengemaa sana, pia ni miradi inayoenda kuinua ukanda huo, kwa kufungua fursa na kuwanyanyua wananchi wa maeneo hayo kwa kasi kubwa, kupitia mnyororo wa thamani, hata kuacha msukumo changamoto kwa wakazi husika kuchangamkia fursa zuinazojitokeza kwa ajili yao na taifa kwa jumla.

**SAFARI YA MABORESHO**

Kabla ya kufikia hatua iliyopo ya utiaji saini, suala la utafiti

INAENDELEA UK.14

BIASHARA

# 'Kuchumbia mazao' na ujazo wa lumbesa unavyodhulumu jasho la mkulima shamba

**Na Beatrice Moses**

"KIKULACHO kipo nguoni mwako. Ni msemo wa wahenga unaodhihirika kwenye maisha ya wakulima kadhaa nchini, kwani licha ya kukabiliwa na hali ngumu wakati wa kulima, kupanda, kuvuna hadi kwenye mauzo, wamejikuta wakiwekewa mitego au masharti magumu na watu ambao wanawaamini,"anasema.

Miongoni mwao ni wanaowalaghai wakulima, kuwalimisha au kuwatega, hata inayofanywa na baadhi ya watu wamejiweka karibu yao, wakiwamo madalali wa mazao na wakala wa pembejeo za kilimo, wanaotumia nafasi zao kugandamiza, hivyo kukwamisha wakulima katika juhudi za kujikomboa kiuchumi.

Kwa miaka kadhaa, imeshuhudiwa uchukuzi wa mazao katika mtindo wa kujazwa na 'kusukwasukwa' maarufu lumbesa. Pia, kuna mtindo mwingine unatajwa wa kuwashawishi kuuza mazao yangali shambani,umaarufu wake kuchumbia, nao unashika kasi. Ni miongoni mwa yanayoingia katika hesabu ya kuwadidimiza wakulima.

Awali mtindo huo maarufu 'kuchumbia' mazao, ulitajwa kushamiri mkoani Mbeya katika wilaya za Kyela, uliofanywa katika kununua mpunga ukiwa shambani. Kwa kiasi kikubwa, ni wafanyabishara kutoka maeneo ya mbali, ikiwamo visiwani Zanzibar wanaovutiwa na ubora wa mchele utokao eneo hilo.

Sasa, ni staili ya biashara kati ya wazalishaji shambani na wafanyabiashara ambao baada ya muda mfupi, ikabainika kuingizwa kwenye baadhi ya vijiji vya wilayani Rungwe na hususani ndani ya Halmashauri ya Busokelo, ambako uzalishaji chakula uko juu.

Viongozi wa ngazi tofauti, tayari wameshayaona hayo na kujitokeza kukemea pamoja, wakisisitiza kwamba maofisa kilimo wanaendelea kutoa elimu kwa wakulima kuhusu kilimo na soko la mazao yao kwa ujumla, ikiwa ni hatua ya kuhakikisha wanavuna kipato kizuri kulingana na walivyolima.



Moja ya masoko mapya yanayojengwa na Halmashauri ya Busokelo, kusaidia wakulima, vilevile kudhibiti 'kuchumbia mazao.' **PICHA ZOTE: MTANDAO**

> **Kununua mazao kwa kuchumbia hairuhusiwi, hivyo Halmashauri baada ya kubaini hilo mwaka jana, ilitoa elimu na kuwasisitiza maofisa ugavi na watendaji wote kufuatilia jambo hilo.**



Hali halisi ya ndizi inayozalishwa katika Halmashauri ya Busokelo, wilayani Rungwe, ambako kunaelezwa kuwapo tabia ya 'kuchumbia' mazao.

### DED NA WAKAZI

Nipashe imeongea hivi karibuni na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo, Loema Peter, anayesema kuwa taarifa za wakulima kushawishiwa na kuuza mazao kwa kuchumbiwa walizipata, wakitambua ni jambo baya wakachukua jukumu la kuzungumza na wananchi kupitia mikutano kadhaa.

"Kununua mazao kwa kuchumbia hairuhusiwi, hivyo Halmashauri baada ya kubaini hilo mwaka jana, ilitoa elimu na kuwasisitiza maofisa ugavi na watendaji wote kufuatilia jambo hilo," anasema.

Mkurugenzi huyo anabainisha kuwa bado wakulima wanafanya anachokiita ukaidi, wakikubali kuuza mazao kwa mtindo huo, akishauri ni vema wakatambua wanajiumiza wenyewe.

Anasema kuna masoko maalum ya mazao ambayo serikali inahamasisha uuzaji mazao kwenye masoko hayo na kuna bei mahsusi zinazoeleweka.

"Nafikiri kuna wakulima au pengine mmoja mmoja ambao kutokana na tabia zao, wana matumizi mabaya ikiwamo ulevi, hivyo pengine ndiyo inawachochea kuuza mazao tofauti na mwongozo waliopewa," anasema.

Mkazi wa Busokelo, Iga Mwakyoma, anasema uuzaji huo wa mazao upo na unatumiwa na watu wenye ushawishi, kama vile madalali.

Mwakyoma anasema, wakulima wanaoshawishiwa wengi ni kutokana na kukabiliwa na hali ngumu ya maisha, hivyo wakionyeshwa fedha wanakubali kuuza mazao yao, pasipo kujali hatima ya kesho inakoelekea.

Inabanishwa kuwa, mtindo huo umewagharimu baadhi ya watu mwaka jana, kwani waliwashawishi kuuza mahindi kwa debe shilingi 6,000, lakini baada ya miezi miwili, kulikuwapo uhaba wa mahindi ambao hadi wakulima wakajikuta, wakilazimika kununua mahindi kwa debe bei shilingi 22,000.

"Ni kujiongezea hali ngumu ya maisha kwenye familia, mfano mtu anauza ndizi ingali shambani, anatumia fedha inakwisha, ndizi ndiyo imekomaa. Anashindwa hata kukata ya kula na familia yake wanabaki kuteseka kwa njaa," anasema mkazi mwingine wa eneo hilo anayejitambulisha kwa jina, Mama Doto.

### MARUFUKU ZILIZOPITA

Mnamo Aprili 2014, aliyekuwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, Christopher Chiza, alitangaza marufuku kwa mtindo huo wa' kuchumbia mazao shambani' akitoa sababu ni kitendo kinachomkosesha mkulima na serikali mapato wanayostahili.

Chiza akatamka hayo wakati wa ziara yake ya kukagua ujenzi wa soko la kimataifa Njiapanda Himo, mkoani Kilimanjaro, akibainisha kuwa 'kuchumbia mazao' shambani kunawakosesha kipato wakulima kwa kuwa, yakivunwa kwa utaratibu mzuri na kuwekwa kwenye soko, ni wazi yanakuwa na kiwango kikubwa cha bei inayompa mlimaji faida.

Pia, katika mwendelezo wa hatua hizo ikaripotiwa miaka miwili baadaye, Julai 2, 2016, habari ambazo pia zikachapishwa kwenye gazeti hili, zilibainisha serikali wilayani Rungwe kuanza ujenzi wa soko la ndizi katika kata ya Lupata, ambako kunapatikana Halmashauri ya Busokelo.

Ni hatua iliyotajwa kulenga udhibiti wa ununuzi wa mazao yakiwa shambani, Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Busokelo wakati huo, Gideon Mapunda, akibainisha ni uamuzi uliotazamiwa kuwasaidia wakulima wa ndizi, mahali hapo kunakolimwa kwa wingi, mazao yote yafike sokoni na siyo kuondokea shambani kwa bei ndogo.

Aprili 3 mwaka huu, kukatangazwa kwenye vyombo vya habari, Mkuu wa Wilaya ya Songea, mkoani Ruvuma, William Ndile, alivyopiga marufuku wafanyabiashara wa ndani na nje ya eneo hilo kununua mahindi ya wakulima yakiwa shambani.

Mkuu wa Wilaya huyo, alitangaza marufuku hiyo kwenye uzinduzi wa mbegu bora za mahindi, akitumia nafasi hiyo kuwaonya wakulima kuacha kuuza mahindi shambani kwa kuwa ununuzi wa mtindo huo ni 'ulanguzi.'


Ndile akafafanua kuwa baadhi ya wakulima pia walipata hasara mwaka jana, baada ya wanunuzi wa mahindi kutoa malipo ya bandia, hata akawaagiza viongozi wa serikali za vijiji na wakurugenzi wa halmashauri ya wilaya hiyo kuhakikisha wanawadhibiti wafanyabishara wanaojipitisha kununua mazao kwa wakulima bila kufuata taratibu.

Ni aina ya utaratibu unaofanywa kienyeji, huku kukiwapo mtindo kwenye mikoa mingi wanunuzi hao wana lingine la ziada, kujaza mizigo yao kwa mtindo uitwao 'lumbesa.'

Hili linafanyika, huku sheria ya kupiga marufuku upakiaji wa mazao na bidhaa kupita ujazo au uzito maarufu 'lumbesa' katika magunia ipo tangu mwaka 2016.

TAFAKURI YA MLALAHOI

# Maradhi ya bodaboda, daladala yanapoambukiza askari trafiki






**NA JOSEPH KULANGWA**
**(+255) 713 410008**
**kulangwasos@gmail.com**

SIKU moja asubuhi naamka sijisikii vema, narudi kulala. Mama anaamka haoni mtu wa kuamka kwenda shule. Niko darasa la pili hapo.

Mara nasikia mtu ananivuta kidole cha mguu. Ni mama, ananiuliza kwanini sijaamka kujiandaa na shule! Namjibu sijisikii vizuri. Anahisi namdanganya. Anamaka: "We Bichwa, niondolee maskhara yako hapa. Amka unawe uende shule."

Enzi hizo majina ya utani tuliyopewa na ndugu na jamaa, yalikuwa ya ajabu ajabutu. Naitwa Bichwa, mwingine Meno, mara Kitumbo au Kichogo. Ili mradi ndiyo yalikuwa majina ya utani.

Tuliyakataa, lakini unafanyaje, ikabidi kukubali tu ukiitwa hivyo nawe unaitika ingawa ulikuwa na jina lako. Leo hii, majina ya utani kwa watoto utasikia Ronaldo, Messi na kadhalika, ili mradi yanavutia.

Basi nikamweleza mama naumwa, ikabidi anisogelee na kunigusa shingoni na mashavuni, kweli akahisi nina joto kali mwilini. Akanihurumia na kuniambia nipumzike ili ajiandae twende hospitali.

Lakini, wakati huo akiniandalia uji usio na sukari. Tulishazoea maisha hayo kwa sababu sukari ilikuwa anasa kwetu. Alipokuwa tayari, akaniamsha na kuniogesha maji ya vuguvugu na kuniandalia uji.

Nilipouonja tu nikatapika. Nikamsikia mama akiwaambia ndugu zangu nje: "Bichwa kautapika uji, basi kweli anaumwa huyu! Ngoja tu nimwahishe hospitalini. "

Akamtuma kaka yangu shuleni kuniombea udhuru. Tukaenda hospitali tukakuta foleni kama kawaida, tukajipanga na wagonjwa wenzetu kusubiri kuonana na daktari. Wakati tukiwa mstarini, akapita daktari akijisemea semea mwenyewe.

Nikamshangaa na kumwuliza mama vipi huyu daktari mbona anazungumza mwenyewe, mwezi mchanga au? Mama akanipuuza huku akiniangalia jicho kali kama nini. Mara yule daktaria kapita tena, anajisemesha tu mwenyewe.

Nikamwuliza tena mama. Kumbe naye hakuwa anajua kitu na hakutaka mimi nijue kuwa hajui. Akaona ili kuondokana na kadhia ile, amwulize jirani aliyekaa naye ambaye alikuwa akimfahamu daktari huyo.

Nikasikia kabisa jirani akimjibu mama, kuwa yule daktari anafanya kazi kwenye kitengo cha maradhi ya akili, hivyo ndiyo sababu amezoeana nao naye anaonekana kuwa kama wao, lakini hana matatizo ya akili.

Kwanini yamenijia haya? Nilikuwa nafikiria sana mambo ya barabarani hususan kuhusu matumizi ya vyombo vya moto, nikilenga zaidi madereva wa bodaboda na daladala na tabia zao wawapo barabarani.

Pia, nikiwahusisha na polisi wa usalama barabarani, ambao kila kukicha hukutana na watu hawa ambao sifichi ni wasumbufu kupita kiasi. Hawa ndio wavunja sheria za barabarani wanaoongoza.

Ajali nyingi za barabarani zimekuwa zikichangiwa sana na kada hii ya madereva wa bodaboda na daladala, kwanini? Kwa sababu wanadhani wao ndio wafalme wa barabarani, hawakamatwi na wakikamatwa huachwa huru baada ya kumalizana na askari.

Wa bodaboda hao ndio kabisa, hawavai kofia ngumu, hawaheshimu alama za barabarani kama vivuko vya waenda kwa miguu vya pundamilia, wao mataa ya kuongozea barabarani sawa na jua tu au mwezi au nyota angani, haviwahusu kabisa. Kubeba mishikaki hakuwasumbui!

Ndio wanaoongoza kwa kukatwa miguu hospitalini kutokana na ajali wazipatazo kila iitwayo leo. Tunalijua hilo, lakini hatujali ndiyo kwanza tunawapachika sifa zama ofisa usafirishaji. Mimi nawaita maofisa ajali.

Kama alivyo yule daktari wa wenye shida ya akili, kama walivyo walimu wa chekechea, naona askari wetu wa barabarani nao wameamua kufanana na madereva wa bodaboda na daladala, wameamua kuzoea na na kuendana nao kiakili.

Wanawaona wakivunja sheria, lakini wanawafumbia macho na kama wakiwasimamisha, hususan wa daladala, watazunguka nao nyuma na kumalizana nao, na kusahau kuwa mchelea mwana kulia hulia yeye.

Wanasahau kuwa kuwaendekeza watu hao ni kusababisha taifa lipate maafa yatokanayo na ajali na kupoteza nguvukazi yake. Sijui kama wenzetu hawa wanaliona hilo au tatizo ni 'Tumbo Street!' Tunasikia tu ukaguzi wa vyeti vya udereva unakuja.

Sina hakika kama ukaguzi huu utahusu madereva wa daladala na bodaboda.

Alamsiki!

# Mkataba alioshuhudia Samia, kupaisha uchumi nchini kwa mtaji Sh. trilioni 1.6

**INATOKA UK.11**

wa madini hayo lilianza mwaka 2000 na sasa mchakato ulikofika ni kufanikisha ajenda za kuingiza wawekezaji wanaohusika moja kwa moja, kuchakata na kufungua viwanda mbalimbali, kwa maslahi ya nchi.

Pia, inatajwa ngazi ya faida nyingine itakayopatikana kwenye uendeshaji huo, ni taifa kunufaika na kodi, ajira kwa wananchi, pia huduma za kijamii. Kinachihomizwa sasa ni kwa Watanzania kuitumia fursa hiyo ya uzalishaji madini kwa mustakabali wa manufaa kwao.

Kupitia utafiti uliofanyika tangu mwaka 2000, mikoa ya Lindi na Morogoro inatajwa ipo katika ukanda wa madini Kinywe, huku mkoa Songwe una madini adimu. Utekelezaji wa mradi unatarajiwa kujikita katika eneo la Ilalo mkoani Lindi, Ngwala wilayani Songwe, pia Ulanga, mkoani Morogoro.

Hadi sasa utafiti unaonyesha kuna jumla ya tani milioni 67 zenye wastani wa asilimia 5.4 ya madini ya kinywe yaliyogundulika katika kijiji cha Chilalo, yanayotarajiwa kuchimbwa kwa miaka zaidi ya 18, huku kijiji cha Ipanko kukigunduliwa tani milioni 63 zenye wastani wa asilimia 7.6 ya madini hayo ya kinywe, yatakayochimbwa kwa miaka zaidi ya 18.

### KAMATI YA MADINI

Mwenyekiti wa Kamati Maalumu ya Majadiliano ya Rais, Profesa Palamagamba Kabudi, anasema kampuni mbili za uchimbaji zimeipatia serikali asilimia 16 ya hisa zisizofifishwa.

"Tunatarajia thamani ya mauzo ghafi ya madini ya kinywe itakuwa Dola za Marekani Bilioni 1.860 na mwekezaji atapata Dola milioni 389, sawa na asilimia 47, huku Tanzania ikivuna Dola milioni 437 sawa na asilimia 53," anasema mwanasheria, Profesa Kabudi.

Kampuni nyingine itakayowekeza kwenye mradi huo wa uchimbaji madini ya kinywe, ni Evolution Energy Limited itakayowekeza Chilalo wilayani Ruangwa mkoani Lindi, kupitia kampuni ya ubia ya Mnyama Kudu Graphite.

Taarifa pia zinaonyesha, serikali itavuna asilimia 51 huku wawekezaji wakisalia na asilimia 41, ambayo gharama za uwekezaji huo zikifikia Dola za Marekani milioni 127.7.

Awali wakati anazungumzia fursa hizo na uendeshaji mzima wa sekta ya madini, Waziri Biteko, anasema mafanikio yanayoonekana sasa kwenye wizara yao, yanatokana na heshima na usimamizi mzuri kutoka kwa Rais Dk. Samia.

"Sisi kama wizara tutaendelea kufanya kazi kubwa ili kulinda thamani ya madini yetu tukiamini kuwa tutafikisha malengo tuliyopewa ya asilimia 10 ya pato la Taifa ifikapo mwaka 2025 kama ilivyoainishwa pia kwenye ilani ya Chama Cha Mapinduzi," anasema Biteko.

BIASHARA

JENNIFER SHIGOLI

# Kahitimu sheria akaweka cheti pembeni, kazama kwenye ujasiriamali 'njia nyeupe'

**Na Elizabeth Zaya**

"Mara baada ya kuhitimu shahada yangu ya kwanza ya sheria mwaka 2012, nilianza kutafuta ajira huku na huku bila mafanikio na kwa sababu hata wakati nasoma, nilikuwa nafanya biashara ndogondogo, nikaamua nijiajiri mwenyewe." Ni maneno ya Jennifer Shigoli, Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Mafunzo ya Ufundi(Arizona), kilichopo Mikocheni, Dar es Salaam.

"Kabla sijaenda chuo, nilikuwa na biashara ya kufanya usafi kwenye majumba na kuuza bidhaa za urembo. Kwa hiyo, nilikuwa na uzoefu kidogo na biashara. Nilipohitimu chuo nikaanza kutafuta kazi bila mafanikio, nikarudi nyuma nikatafakari hivi mbona kabla ya hapo nilikuwa nafanya shughuli zangu, kwa nini nisifanye?

"Kwa hiyo, nikaamua kurudi kwenye kazi yangu ile ya mwanzo ya kufanya usafi majumbani. Awali, nilikuwa nanunua bidhaa za kufanya usafi madukani, lakini nikaamua kwenda kusomea namna ya kutengeneza mwenyewe na nilifanikiwa kufanya hivyo. Kwa hiyo ikanirahisishia kufanya shughuli zangu hizo za usafi kwa kutumia bidhaa zangu mwenyewe."

Anasema, ili kuboresha bidhaa zake, alijifunza namna ya kuziwekea lebo zenye viwango, jambo lililomtambulisha zaidi kwa wateja wake na kukubalika zaidi.

"Hii ndio changamoto kubwa kwa wajasiriamali, wengi wanashindwa kuboresha bidhaa zao na hivyo kujikuta wanashindwa kusonga mbele. Niliiona hilo kabla, wateja walikuwa wanasita kutumia bidhaa zangu, kwa sababu hiyo. Lakini, baada ya kuweka lebo, nilianza kupata mapokezi tofauti, walianza kuzikubali zaidi na kuniamini na hapo ndipo kazi zilianza 'kuchanganya'.

"Nakumbuka tenda kubwa ya kwanza kwangu nilipata kwenye hoteli moja ya Sinza (Dar es Salaam) Sh.815, 000 na ili wanione niko 'serious' (makini), siku ya kupeleka bidhaa zangu, nikasema nisifanye kinyonge , nikakodi 'kirikuu' (gari dogo la mizigo).

"Nikachukua na stika zangu nikazibandika. Nilifanya hivyo, kwa sababu niligundua kwamba namna unavyojiweka ndivyo na watu wanavyokuchukulia. Kwa hiyo, safari yangu ya kuzalisha ilianzia pale, niliendelea kukutana na tenda nyingine nyingi," anasimulia Jennifer.

Anasema kuboresha zaidi kazi zake, akaendelea kusaka ujuzi sehemu za ndani na nje ya nchi, hata kumwezesha kuanzisha mafunzo kwa wajasiriamali wengine, hususani katika namna ya kuboresha bidhaa zao na kuchangamkia fursa za masoko.

"Watu walikuwa wanatoka mikoani kuja kufuata mafunzo Dar es Salaam, au wakati mwingine walikuwa wananiita naenda kuwafundisha huko waliko. Kupitia kazi zangu hizo, ndipo nilizidi kukutana na watu na kubadilishana nao uzoefu, ikiwamo namna ya kuingia katika uzalishaji mkubwa," anasema.

"Mwaka 2014/015, nilianzisha kampeni nyingine inayoitwa 'Choo Salama', lengo lilikuwa kwenda shuleni kufanya usafi kwa kutumia bidhaa zangu mwenyewe. Nilifanya vile bila ya kuwatoza gharama yoyote, nikiamini watoto wakienda majumbani kwao watawaambia wazazi wao.

"Kupitia kampeni hiyo, nikaongeza wadau wengine wakiwamo Taasisi ya Walimu Wanawake ambao walinishika mkono, tukazunguka kwenye shule nyingi na nikawa nawafundisha namna ya kufanya usafi na wakawa wanapenda bidhaa zangu. Wazazi wao wote waligeuka na kuwa wateja wangu," anasimulia.

Anafafanua kwamba, alipozunguka kwenye kampeni zake shuleni, alibaini kuwapo fursa nyingine ya kutengeneza bidhaa za hedhi, baada ya kukutana na wanafunzi waliokuwa wanashindwa kwenda shuleni kila wanapoingia kwenye hali hiyo.

"Kwa hiyo baada ya kufanya utafiti wa kutosha nikaanza kutengeneza taulo na pia kufundisha wengine," anaeleza





Wanafunzi katika Chuo cha Arizona, Dar es Salaam. Picha ndogo, Mkurugenzi Mtendaji wa chuo hicho, Jennifer Shigoli. **PICHA ZOTE: ELIZABETH ZAYA**

**ALIVYOASISI CHUO**

Mwaka 2019 akasajili chuo chake kiitwacho Arizona, kinachojikita zaidi katika mafunzo kwa vitendo, akisema lengo ni kumfundisha mtu anapohitimu, anakuwa na uwezo kutengeneza cha kwake, akisisitiza "sikutaka eti mtu anatoka hapa halafu anaenda tena kwenda kutafuta sehemu nyingine ya mafunzo."

Anasema, hadi sasa chuo kinatoa mafunzo ya kutengeneza sabuni, ushonaji, upishi, kutengeneza keki, vipodozi, kujifunza kiingereza, kompyuta, upambaji, urembo na elimu ya ujasiriamali.

Mama huyo anasema zaidi ya wanafunzi 3000 wamepata mafunzo katika chuo hicho tangu kianzishwe, wakitoka nchini, pia Jamhuri ya Kidemkrasia ya Congo (DRC), Comoro, Burundi na Burkinafaso.

Jennifer anasema asilimia 60 ya wanafunzi waliopita chuoni hapo, wako kazini wengi wameojiajiri, akitaja aina ya mafunzo wanayotoa ni ya muda mfupi, kati ya mwezi mmoja na mitatu, kwa sababu imezama zaidi katika mustakabali wa vitendo zaidi. Anaelzea, kozi zinazochukua wanafunzi wengi ni za kutengeneza vipodozi na bidhaa za nywele, ushonaji na kubuni mitindo na mapishi.

> "Mimi mtu anayetoka hapa na kwenda kuajiri hata mtu mmoja, namheshimu sana. Naamini ndoto yangu niliyokuwa naota ya kuwa sehemu ya kutatua matatizo ya watu imeanza kutimia.

Pia, anataja kuwapo mradi mahsusi uitwao 'amka' ambao lengo lake ni kuasaidia kulipa ada kwa wasiojiweza.

**NJIA ALIKOPITA**

Jeniffer anaeleza njia alikopita, wakati anaanza ujasiriamali hakupokelewa vizuri na watu, wakiwamo ndugu zake, kwa sababu wengi walitarajia baada ya kusoma, angefanya kazi za kisheria, eneo la taaluma yake.

"Kwa miaka michache hii ambayo nimefanya kazi kwenye chuo hiki tangu tukifungue, ninaona matunda yake, si kwangu tu lakini kwa namna ambavyo tumetengeneza ajira za watu waliopitia kwetu na hilo ndilo la msingi zaidi.

"Mwanafunzi amekuja hapa mwaka 2020, lakini mpaka sasa amefungua kiwanda na ameajiri watu zaidi ya 30. Kuna mwingine yuko hapa Mikocheni (Dar es Salaam ) amefungua duka kubwa la vipodozi anavyovitengeneza mwenyewe. Wapo wengi wamejiajiri kwa sasa waliopita hapa, hili ni jambo jema na la kujivunia.

"Mimi mtu anayetoka hapa na kwenda kuajiri hata mtu mmoja, namheshimu sana. Naamini ndoto yangu niliyokuwa naota ya kuwa sehemu ya kutatua matatizo ya watu imeanza kutimia," anasema

**UJUMBE WAKE**

Anasema kila ujuzi au taaluma aliyo nayo mtu, anaweza kutumia katika shughuli za ki-ujasirimali na si kusubiri aajiriwe.

"Ajira siyo mbaya, lakini na ujasiriamali ni mtizamo. Watu wengi ukiwaambia wewe ni mjasiriamali, wanakuuliza unafuga kuku, au unalima? Watu wanatakiwa kufahamu kuwa, katika kila sekta au taaluma aliyonayo mtu kuna ujasiriamali.

"Elimu yoyote aliyonayo mtu, ni mtaji tosha. Siyo lazima utoke kwenye taaluma yako, watu wafunguke na kutanua mawazo yao. Mtu asiweke akilini kwamba kazi ni mpaka akakae ofisini, hapana! Unaweza kujiajiri kwa kutoa huduma kupitia taaluma au ujuzi ulionao," anasema.

Anasema kabla ya kuanza ujasiriamali, alitegemea sana, lakini baada ya kuanza shughuli za kijasiriamali, kumemkomboa kiuchumi akiwa na kipato binafsi na familia yake, vilevile akisaidia wengine.

Mama huyia anasema malengo yake makubwa, ni kuanzisha kiwanda kikubwa mkoani Pwani katika eneo la Zegeleni, ambako amewekeza ardhi, hata kuifanyaArizona kuwa kituo kikubwa barani Afrika cha kutoa ujuzi kwa makundi yote.



## RC aagiza upangaji bei za maji zisizoumiza wananchi

**Na Thobias Mwanakatwe,**
ITIGI

MKUU wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, ameziagiza jumuiya za maji mkoani hapa kupanga bei za maji kulingana na gharama za uzalishaji ambazo haziwakomoi wananchi.

Alitoa agizo hilo juzi wakati akizungumza na wananchi wa Kijiji cha Kihanju Halmashauri ya Itigi wilayani Manyoni baada ya kuukabidhi mradi wa maji kwa jumuiya ya maji uliojengwa kwa ufadhili wa Kampuni ya Vinywaji Serengeti (SBL) kwa gharama ya Sh.milioni 293.

Serukamba alisema jumuiya za maji zinatakiwa kupanga bei za maji ambazo ni rafiki kwa wananchi ili waendelee kufurahia huduma kwani serikali inataka kuhakikisha wananchi wote wa mjini na vijijini wanapata maji.

Alisema wananchi washiriki katika shughuli zote za uendeshaji na matengenezo kwa kushirikiana na jumuiya ya maji ambacho ni chombo kilichoundwa na wananchi wenyewe chini ya Sheria Mamba 5 ya Maji na Usafi wa Mazingira ya mwaka 2019.

Serukamba alisema Sera ya Maji ya mwaka 2002 inatoa majukumu kwa wananchi kulipia gharama za huduma za maji, kutunza vyanzo vya maji visikauke na kulinda rasilimali za miundombinu ya maji kama vile mabomba na mitambo ya kusukuma maji.

Aidha, Mkuu wa Mkoa alilishukuru Shirika la Water Aid Tanzania na Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) kwa kutekeleza na kukamilisha ujenzi wa mradi huu.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya SBL, Mark Ocitti alisema mradi huo umegharimu Sh. milioni 293.1 na utahudumia wakazi zaidi ya 2,000.

Alisema sekta ya kilimo katika maeneo hayo inategemewa kukuwa kwa kiasi kikubwa kwakuwa kutakuwa na maji lakini pia uwepo wa muda wa kutosha ambapo mashirika mbalimbali yatafanya uwekezaji kuongezeka.

Meneja wa RUWASA Wilaya ya Manyoni, Mhandis Gabriel Ngongi alisema katika bajeti ya mwaka huu mamlaka imetenga Sh.milioni 30 kwa ajili ya kupeleka maji katika vijiji vingine vitatu kutokea mradi ulipo.

# Utafiti wabaini aina 25 ya mbegu bora za mazao

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

TAASISI ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) imegundua aina 25 za mbegu bora za mazao ambazo zimeidhinishwa kutumiwa na wakulima nchini.

Mkurugenzi Mkuu wa TARI, Dk. Geofrey Mkamilo, alibainisha hayo juzi wakati akizungumza na Nipashe kuhusu utafiti wa kilimo waliyoufanya kupitia vituo vyake.

Dk. Mkamilo alisema aina hizo za mbegu ambazo tayari zimeidhinishwa na Taasisi ya Uthibiti wa Ubora wa Mbegu Tanzania (TOSCI) ni mtama (aina mbili), migomba (aina nne), viazi vitamu (aina mbili), miwa (aina sita), maharagwe (aina sita), ngano (aina mbili), choroko (aina mbili) na aina moja ya mpunga.

Dk. Mkamilo alisema kuwa aina hizo za mbegu zinastahimili ukame na magonjwa na kwamba zina uwezo mkubwa wa kutoa mazao mengi pindi zinapotumika katika msimu wa kilimo kwenye maeneo mbalimbali hapa nchini.

Hata hivyo alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuweka mkazo katika kuisaidia taasisi kupanua wigo wa kufanya utafiti mbalimbali za mbegu ambazo zinawasaidia wakulima kuendesha kilimo chenye tija kinachowapa matokeo chanya wao na taifa kwa ujumla.

"Mfano mbegu za ngano tulizozivumbua zina asilimia 38.9 ya gluneti, protini inayohitajika sana katika viwanda vya uzalishaji, na zina uwezo wa kuzalisha kati ya tani nne hadi 4.6 kwa hekta," alieleza Dk. Mkamilo.

Aidha, alisema pia kwa mara ya kwanza TARI imefanikiwa kugundua na kuzalisha mbegu za miwa zenye uwezo wa kuzalishwa kwa kutegemea mvua, ambapo alisema hatua hiyo itawasaidia wakulima wadogo kupunguza gharama za uzalishaji ikilinganishwa na mbegu za awali zinazotegemea maji ya umwagiliaji kwa asilimia 100.

Mbali na hilo Dk. Mkamilo alisema katika tafiti zao nyingine walizofanya wamefanikiwa kugundua nafasi mpya ya kupanda pamba, ambayo ni sentimita 60 kwa sentimita 30, huku akisisitiza hatua hiyo ni muhimu na imechochea ongezeko la mavuno kutoka wastani wa kilo 710 hadi 1, 422 kwa ekari moja.

Dk. Mkamilo alifafanua kuwa katika juhudi za kuongeza tija ya uzalishaji wa zao la pamba nchini, TARI imefanya utafiti na kugundua zana rahisi ya kupandia pamba yenye uwezo wa kupanda ekari moja kwa saa moja hadi saa tatu, badala ya saa 11 kwa kutumia jembe la mkono.

Katika hatua nyingine Dk. Mkamilo alisema TARI imeongeza uzalishaji wa mbegu bora kutoka tani 481,23 mwaka 2020/21 hadi kufikia tani 1,225.872 mwaka 2021/2022, ambapo alisema uzalishaji wa miche, vikonyo, pingili umeongezeka kutoka 7,998, 784 kwa mwaka 2021/22 hadi kufikia 19,822,349 kwa mwaka 2023 katika mazao ya parachichi, michikichi, mihogo, miwa, viazi mviringo, korosho, matunda na viungo.

Aliongeza kusema ili kuhakikisha matokeo ya utafiti yanaleta mabadiliko chanya kwenye sekta ya kilimo nchini,Dk Mkamilo alisema taasisi hiyo imefanikiwa kupeleka matokeo ya utafiti mbalimbali kwa wadau wapatao 5,497,547 wakiwemo wakulima, maofisa ugani pamoja na wadau wengine husika.

Alisema njia zilizotumika kusambaza teknolojia hizo ni pamoja na maonyesho mbalimbali ya wakulima, maonyesho ya kilimo biashara, mafunzo wezeshi, majukwaa bunifu pamoja na mashamba darasa.



Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson (wa pili kulia), akikabidhi msaada ya vyakula kwa Mkurugenzi wa kituo cha watoto yatima cha Alhaafidhu Islamic Kondoa Ukh – Ti, Aisha Nobbe baada ya kuhitimisha mashindano ya Quran katika Msikiti Mkuu wa Gadaffi jijini Dodoma juzi. Wa (tatu kulia) ni Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule. **PICHA: PETER MKWAVILA.**

# TEA yatumia mil.750/- ujenzi shule ya kiingereza

**Na Joseph Mwendapole,**
DODOMA

MAMKLAKA ya Elimu Tanzania (TEA), imejenga shule ya mchepuo wa kingereza mkoani Dodoma kwa Sh. milioni 750 ambayo iko Kata ya Makulu mkoani hapa.

Akizungumza na waandishi wa habari waliotembelea shule hiyo juzi, Mkuu wa shule hiyo, Dina Mndasha alisema ilianza rasmi Januari mwaka huu na ina wanafunzi 215.

Alisema shule hiyo ambayo inafundisha kwa lugha ya kingereza ni ya serikali na kwamba wameanza na wanafunzi wa darasa la awali hadi wa darasa la tatu.

Alisema kwa sasa vyumba nane vya shule hiyo vimekamilika na sita vinatumika kwa ajili ya kufundishia, kimoja kinatumika kama bwalo la chakula wakati kingine kinatumika kwa ajili ya kupumzikia.

"Mwitikio ni mkubwa sana mahitaji yamekuwa mengi sana tunapata maombi mengi ya kujiunga na shule hii lakini bado miundombinu haitoshelezi. Ada ya shule hii ni ndogo sana ndiyo sababu watu wengi wanaihitaji," alisema

Alisema wamekuwa wakiwapa motisha walimu wa shule hiyo wanaofaulisha ambapo wanaopata alama A hupewa motisha wa Sh. 10,000 na kwamba wanafanya hivyo ili wanafunzi wafaulu kwa daraja la juu. Alisema ili kupima ufundishaji wa walimu wa shule hiyo wamekuwa wakiagiza mitihani ya kila mwezi kutoka shule zingine za mchepuo wa kingereza kutoka jijini Dar es Salaam.

Alisema Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma amepeleka walimu kwenye shule hiyo na ameahidi kujenga uzio hali ambayo itawahakikishia usalama.

Alimpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa uwekezaji anaoufanya kwenye elimu kwa kuweka fedha nyingi ambazo zimesaidia kwa kiasi kikubwa kujenga miundombinu ya elimu.

Alisema shule hiyo haibagui na inapokea wanafunzi wenye mahitaji maalum ambao wanasoma mchanganyiko na wanafunzi wengine wasio na mahitaji maalum.

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano, Mamlaka ya Elimu Tanzania, Bestina Magutu alisema shule hiyo imejengwa kupitia mfuko wa elimu unaosimamiwa na TEA.

Alisema serikali ya awamu ya sita imeendelea kuupa fedha mfuko wa elimu hali ambayo imewezesha TEA kujenga miundombinu kwenye shule za msingi na sekondari. Alisema mpaka sasa mfuko wa elimu umeshatoa ufadhili wenye wa Sh.bilioni 3.6 kwenye miradi ya elimu katika shule za msingi na sekondari Mkoa wa Dodoma.





# RC aagiza kufanyika operesheni kamata madereva watoto

Na Grace Mwakalinga,
MBEYA

SERIKALI ya Mkoa wa Mbeya imeagiza Kikosi cha Usalama Barabarani kuanza operesheni ya kukagua leseni za madereva bajaji na bodaboda ili kukabiliana na wimbi la watoto kuendesha vyombo hivyo na kusababisha ajali.

Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Beno Malisa alitoa agizo hilo jana wakati wa kilele cha maadhimisho ya wiki ya nenda kwa usalama barabarani, ambayo yalihitimishwa eneo la Stendi ya Kabwe jijini Mbeya.

Malisa aliomba ukaguzi wa leseni uanze mara moja kuanzia majira ya saa 12 jioni ili kuwakamata watoto ambao wamejiingiza kwenye udereva pasipokuwa na leseni hali inayohatarisha maisha ya watumiaji wengine wa barabara.

"Kwa uchunguzi wangu niliobaini nimeona idadi kubwa ya watoto kuendesha bajaji na bodaboda, sasa hali hiyo ni kinyume na sheria za usalama barabarani, naomba Jeshi la Polisi muanze operesheni ya kukagua leseni ili kuangalia ukubwa wa tatizo hili ambalo linasababisha kero barabarani," alisema Malisa.

Aidha, aliwataka madereva kuzingatia sheria za usalama barabarani ili kukabiliana na wimbi la ajali ambalo kwa muda mrefu limekuwa likiusumbua Mkoa wa Mbeya.

Kamanda wa Kikosi cha Usalama barabarani, Mkoa wa Mbeya, Yusuph Kamotta alisema miongoni mwa vyanzo vya ajali mkoani humo vinasababishwa na makosa ya kibinadamu ikiwemo mwendo kasi, uchovu, msongo wa mawazo.

Alisema vyanzo vingine ni ubovu wa magari na kuwasihi madereva kutokubali kuendesha vyombo vya moto vibovu hata kama wanalazimishwa na mabosi zao badala yake watoe taarifa za siri kwa polisi ili kuyakamata magari ya namna hiyo. "Pia kuna tatizo cha wananchi kutozingatia sheria za usalama barabarani na badala yake kuvuka kwenye maeneo yasiyokuwa rasmi na kusababisha ajali lakini pia madereva wengi kutokuwa na elimu ya matumizi ya alama za usalama barabarani," alisema Kamanda Kamotta.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi wa Polisi, ACP Benjamin Kuzaga, aliwataka wananchi kuacha tabia ya wizi wa vifaa vya usalama barabarani.

Alisema kumekuwa na tatizo kwa baadhi ya wananchi kung'oa alama za barabarani na kwenda kuviuza kama vyuma chakavu hali inayokwamisha jitihada za serikali katika kuwalinda wananchi wake dhidi ya ajali.

Hivyo, aliwataka wananchi kuacha tabia hiyo mara moja na kwamba atakayebainika atachukuliwa hatua kali kwa mujibu wa sheria kwa sababu atakuwa akihujumu miondombinu iliyojengwa na serikali.

Mwenyekiti wa Kamati ya Usalama Barabarani Mkoa wa Mbeya, Rajab Bulogo alisema katika maadhimisho ya wiki ya nenda kwa usalama barabarani iliyoanza April 12 hadi 20 zaidi ya madereva 700 wamepata mafunzo ya udereva na kutunukiwa vyeti vya mafunzo.



Ofisa Mkuu wa TEHAMA kutoka Wizara ya Afya, Jackson Shayo (kushoto), akitoa maelezo kwa Kaimu Katibu Tawala wa Mkoa wa Mbeya, Ernest Hinju, kuhusu namna kituo cha mawasiliano cha mfumo wa m-mama kitakavyorahisisha upatikanaji wa usafiri wa dharura ili kuokoa maisha ya akinamama wajawazito na watoto wachanga, baada ya uzinduzi wa huduma ya m-mama katika Hospitali ya Rufani ya mkoa huo hivi karibuni, ikiwa ni ushirikiano wa serikali, Vodacom Tanzania Foundation, Pathfinder, Touch Foundation na USAID. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wajane wengi vijijini hawana elimu ya mirathi

Na Grace Mwakalinga,
MBEYA

WANAWAKE wajane mkoani Mbeya wamesema licha ya serikali na wadau kuendelea kutoa elimu ya kisheria kuhusu haki zao, lakini bado kuna kundi kubwa la wajane waishio vijijini hawana elimu ya mirathi.

Wamesema hali hiyo inasababisha wajane hao kupoteza haki zao pindi wanapofiwa na waume zao.

Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Wanawake Wajane Tanzania, Aurelia Kanyengele alitoa kauli hiyo kwenye maandalizi ya mwanamke mjane duniani ambayo kitaifa inatarajiwa kuadhimishwa Juni 23 mwaka huu mkoani Mbeya.

Alisema idadi kubwa ya wanawake wajane wananyanyaswa na kupoteza haki zao za mirathi kutokana na kukosa elimu hali inayosababisha baadhi yao kuishi maisha magumu na watoto wao.

"Kinamama wengi hawajapata elimu ya sheria za mirathi, mwanamke akifiwa na mumewe ndugu wa marehemu wanaanza manyanyaso kwa kutokujua anaanza kuhangaika kuomba kwa watu wasio sahihi," alisema Aurelia.

Mratibu wa Chama cha Wanawake Wajane Tanzania, Daniel Simfukwe alisema wajane wengi wanapofiwa hukosa kujiamini na wengine kupata msongo wa mawazo na kupunguza ufanisi katika utendaji kazi na kusababisha kuyumba kwa familia zao.

# Wizara ya Kilimo yaombwa kutenga fedha uchimbaji mabwawa

Na Grace Mwakalinga,
MBEYA

SERIKALI mkoani Mbeya imeomba Wizara ya Kilimo kutenga fedha kwa ajili ya kuchimba mradi wa mabwawa ya kilimo cha umwagiliaji, ili kunusuru kahawa ambayo iko hatarini kutoweka kutokana na mabadiliko ya tabia nchi.

Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Beno Malisa alitoa ombi hilo jana kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera alipofungua kikao cha wadau na wakulima wa zao hilo kilichoandaliwa na Bodi ya Kahawa Tanzania ( TCB).

Malisa alisema kuwa hali ya uzalishaji katika baadhi ya maeneo sio nzuri sababu kubwa ikitajwa kuwa ni mabadiliko ya tabia nchi ikiwamo uhaba wa mvua, magonjwa na kusababisha asilimia zaidi ya 20 ya miche kukauka.

"Asilimia 20 ya miche kukauka ni kubwa sana hivyo tunaomba Wizara ya Kilimo kwa kushirikiana na bodi ya kahawa muongeze uboreshaji wa kwenye kilimo hiki sambamba na upatikanaji wa masoko ya uhakika nje ya nchi ili mkulima aweze kunufaika," alisema Malisa.

Alisema kuna kila sababu wakulima kupatiwa elimu ya teknolojia za kisasa za uzalishaji ambazo hazitategemea mvua ikiwepo uzalishaji wa miche bora inayoweza kukabiliana na magonjwa na kuwafikia wakulima kupitia AMCOS sambamba na kuwepo kwa bei elekezi.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TCB, Kajiru Kissenge alisema wataimarisha utafiti wa kahawa na kuanzisha mfuko wa pembejeo nchini na masoko ya kahawa.

Ofisa Kilimo Mkoa wa Songw , Semeni Halijuma, alisema wamejipanga kuongeza uzalishaji wa kahawa kutoka tani 12,446 mpaka 32, 617 ifikapo mwaka 2025 pamoja na kuongeza ubora utakaokidhi masoko.

Mkulima Selena Saimon aliomba Bodi ya Kahawa Tanzania (TCB) kuwa na utaratibu wa kutoa taarifa za masoko na bei elekezi mara kwa mara katika soko la dunia ili kuwasaidia kuachana na kampuni ambazo baadhi zimekuwa mwiba kwao.

# Matukio ya ukatili wa kijinsia Zanzibar yapungua

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR.

MATUKIO ya udhalilishaji wa kijinsia yaliyoripotiwa Machi mwaka huu yamepungua hadi kufikia 155 kulinganishwa na Aprili yaliyokuwa 164.

Takwimu hizo zilitolewa jana kwa waandishi wa habari na Ramla Hassan Pandu kutoka Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Kitengo cha Makosa ya Jinai, Madai na Jinsia.

Alisema kati ya matukio hayo yaliyoripotiwa waathirika zaidi ni watoto ambao ni 134, wanawake watu wazima 14 na wanaume saba.

Ramla alisema kati ya matukio hayo, ubakaji yanaongoza ambayo ni 69 yakifuatiwa na ulawiti 29, shambulio 29, kukashifu 14, kuingilia kinyume na maumbile ni sita.

Aidha alisema Wilaya ya Mjini inaongoza kuwa na matukio mengi ikilinganishwa na wilaya zingine kwa kuwa na matukio 43.

"Wilaya ya Kusini Unguja imeripotiwa kuwa na idadi ndogo ya matukio kuliko wilaya zote ambapo matukio mawili"alisema Ramla.

Alisema matukio 125 kati ya 155 yalioripotiwa yapo chini ya upelelezi wa polisi, matukio 26 yapo kwa Mkurugenzi wa Mashtaka, matatu yapo mahakamani na moja limefungwa na polisi.

Mkurugenzi wa Idara ya Jinsia, Wanawake na Watoto, Siti Abasi Ali, alilitaka Jeshi la Polisi kuongeza nguvu ya ulinzi kwa watoto hasa katika kipindi hiki cha Sikukuu ya Idd ambapo wahalifu hutumia mwanya huo kuwadhalilisha watoto.

Aidha, aliwataka wazazi na welezi kuwa na udhibiti wa malezi ya watoto wao na kujua mienendo yao.

Mkurugenzi huyo aliwataka wazazi kuongozana na watoto wao wakati wanapoenda katika viwanja vya kusherehekea sikukuu kwa sababu kipindi hicho vitendo vya udhalilishaji huwa wingi.

"Wazazi tuhakikishe kuwa watoto wetu tunawapa ulinzi mzuri ili kuwakinga na vitendo vya udhalilishaji lakini pia kipindi hiki cha sikukuu watoto wingi hupotea kutokana na kutokua na ulinzi"alisema.

Hata hivyo aliwatahadharisha wazazi kuacha kuwaweka mapambo watoto ambayo hayastahili kwa sababu baadhi ya watoto huwekwa kope za kubandika, manukato ambayo kwa umri wao hawastahiki.

Mrakibu Msaidizi wa Jeshi la Magereza, Zanzibar, Salum Msabah Ali, alisema wafungwa katika Gereza la Zanzibar lina idadi ya watoto wengi ambao wamehukumiwa kwa vitendo vya udhalilishaji.



Waandishi wa habari wakishiriki futari iliyoandaliwa na Jumuiya ya Waandishi wa Habari za Maendeleo Zanzibar (WAHAMAZA), kisiwani humo juzi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN.**

# Waziri aagiza watendaji kushirikiana ili kuongeza ufanisi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda, Omar Said Shaaban, amewataka watendaji wa taasisi zilizo katika wizara hiyo kufanya kazi kwa ushirikiano ili kuongeza ufanisi.

Alieleza hayo wakati wa futari ya pamoja iliyoandaliwa na Taasisi ya Viwango Zanzibar (ZBS) iliyojumuisha watendaji wa taasisi za wizara hiyo na viongozi mbali mbali.

Alisema ili kufikia malengo ya kuwepo kwa taasisi hizo kuna haja ya kufanya kazi kwa pamoja, ubunifu na kujituma kama inavyoonekana katika taasisi hiyo jambo linaoongeza hari na ufanisi kazini.

"Tumekuja hapa kuungana na wenzetu wa ZBS ambao wameonyesha uhalisia wa kazi na majukumu waliyonayo kuwa ni pamoja na kuwaunganisha wadau wa sekta za biashara na viwanda, watendaji wa taasisi nyingine na viongozi wa serikali," alisema.

Mkurugenzi Mkuu wa ZBS, Yussuf Majid, aliwashukuru viongozi wa wizara hiyo na wizara nyingine pamoja na wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa kuendelea kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya serikali katika sekta mbalimbali.

Alisema kuwa taasisi yake inafarajika na msaada inaoupata kutoka serikali kuu jambo linaongeza morali ya utendaji na kuwashukuru wafanyakazi wa taasisi hiyo kwa ushirikiano wanayompa.

"Mafanikio yanayoonekana kwenye taasisi yetu yanatokana na umoja na ushirikiano. Kila mara tunafanya kazi kwa timu chini ya uangalizi wa bodi yetu lakini pia miongozo ya sheria na viongozi wa wizara yetu," alisema Majid.

Hafla hiyo ilitanguliwa na utoaji wa vifaa tiba na usafi kwa Hospitali ya Mnazi Mmoja, kwamba Daktari Bingwa wa magonjwa ya upasuaji, Mwanabaraka Saleh ambaye pia ni Mkurugenzi wa Idara ya Upasuaji hospitalini hapo, alisema wanapokea idadi kubwa ya wajawazito na wagonjwa.

Dk. Mwanabaraka alisema hali hiyo inawapa wakati mgumu katika utekekezaji majukumu yao, hivyo kuchangia vifo vingi vya watoto vinavyochangiwa na wajawazito kutofuata maelekezo ya wataalam wa afya

Alisema kutotumia dawa ipasavyo husababisha vifo, hivyo na kuwataka wananchi kufika hospitali kwa wakati na kufuata maelekezo ya wataalamu wa afya. Akizungumza kwa niaba ya uongozi wa hospitali hiyo, Mkurugenzi Mipango wa hospitali hiyo, Abdalla Khamis Haji, alisema msaada huo utawasaidia kutatua zinazowakabili.

Aidha, alipongeza uamuzi wa taasisi hiyo kutoa msaada huo na kueleza kuwa utasaidia kukabili tatizo linalotokea kutokana na kupokea wagonjwa zaidi ya 100 wa kawaidda na 50 wajawazito wanaofika kujifungua kwa siku. Akikabidhi msaada huo, uliohusisha mashuka, dawa za usafi, mashine ya kupimia presha na vifaa vingine, Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya ZBS, Khadija Ali Sheha, alisema taasisi hiyo imeona haja ya kutumia sehemu ya mapato inayaokusanya kuunga mkono jitihada za serikali kuwasaidia wananchi katika masuali afya.

Aidha, aliwapongeza wafanyakazi wa hospitali hiyo kwa kujituma na kufanya kazi ya kuwahudumia wananchi licha ya mazingira magumu ya kazi yanayochangiwa na idadi kubwa ya wagonjwa wanaohitaji huduma.

# Wizara ya Utalii kuyalinda, kuhifadhi maeneo ya kale

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Utalii na Mambo ya Kale imesema imejipanga kulinda na kuhifadhi maeneo ya kihistoria yaliyopo Unguja na Pemba kwa ajili ya kuingiza kipato na kuvutia watalii.

Hayo yalisemwa jana na Naibu Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Dk. Amina Ameir Issa wakati akiendesha kikao cha pamoja na watendaji wa sekta ya utalii na mambo ya kale katika mikakati ya kukuza sekta ya utalii nchini.

Alisema serikali imewekeza fedha nyingi katika sekta ya utalii ikiwamo ukarabati wa majengo ya kale kwa lengo la kuvutia idadi kubwa ya watalii wanaotembelea na kujua historia yake.

Alisema katika mwaka 2018 maeneo saba ya kihistoria yamefanyiwa ukarabati ikiwamo kutayarisha maelezo ya historia zake hatua ambayo imesaidia wageni kujua umuhimu wake.

Alitayataja maeneo yaliyofanyiwa ukarabati mkubwa ni Khole, Bungi, Mwinyi Mkuu, Dunga, Fukuchani na kwa upande wa Pemba ni Mkamandume na mji wa kale uliozama chini ya bahari Mkumbuu.

Aidha, Mkurugenzi wa Utalii, Dk.Abdalla Mohamed Juma, alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imejikita zaidi katika uwekezaji wa utalii wa kihistoria wa majengo ya kale.

Alisema kwa asilimia 50 watalii wanaokuja nchini hupenda kutembelea majengo yaliyobeba historia ya kale kwa ajili ya kufahamu mambo yaliyofanyika kupitia tawala za kale.

Ofisa Mwandamizi wa Idara ya Makumbusho ya Kale, Omar Ali Machano, alisema wapo katika mipango ya kuyafanyiya ukarabati mahandaki yaliopo Hamamni Mjini Unguja pamoja na Kijificheni na Forodhani.

Mwenyekiti wa Kamisheni ya Utalii Zanzibar, Rahim Mohamed Bhaloo alisema utalii wa makumbusho ya mambo ya kale mahitaji yake ni makubwa ikiwamo wageni na watafiti kufanya kazi za utafiti wa kale wa historia ya Zanzibar.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA PASPORT



**BARAKA CYRUS HEBLING**

Mtajwa hapo juu amepotelewa na passport yenye NO, **TAE 369904** iliyotolewa na ofisi ya uhamiaji tarehe 6 Mwezi Novemba mwaka 2020. Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi **KIL/MOS/RB/132466/2023**

## KUPOTEA KWA VYETI



**ALEXANDER NYARUBAMBA MAIRA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0359/1989** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **KIGURUNYEMBE SEKONDARI** mwaka 1989. Cheti cha kidato cha sita chenye index namba S0310/1991 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **FOREST HILL HIGH SCHOOL** mwaka 1991. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa za polisi: **DAR/BUG/RB/136305/2023.**

## KUPOTEA KWA PASPORT



**ZYUNIROSE DAVDI**

Mtajwa hapo juu amepotelewa na passport yenye NO, **TAE 369299** iliyotolewa na ofisi ya uhamiaji tarehe 4 Mwezi Novemba mwaka 2020. Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi **KIL/MOS/RB/132466/2023**

---

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA YA MULEBA**

**LILILOPO MULEBA MKOA WA KAGERA**

**MAOMBI NA. 50/2022**

**REGISTERED TRUSTEES OF THE ROMAN CATHOLIC CHURCH BUKOBA DIOCESE ............MLETA MAOMBI**

**DHIDI YA**

1. **KITOKO VILLAGE COUNCIL**
2. **PASCHAL RWECHUNGURA ............WAJIBU MAOMBI**

**KWA: 1. KITOKO VILLAGE COUCIL**
**2. PASCHAL RWECHUNGURA (POPOTE PALE ULIPO)**

Mnaarifiwa kuwa maombi Na. 50/2022 yamepangwa kutajwa tarehe 12.05.2023 mbele ya Mwenyekiti wa Baraza, J.K. Banturaki saa 2:30 Asubuhi, mahali – Muleba (Mamlaka ya Mji Mdogo). Hivyo, mnaamriwa kuhudhuria wenyewe/wawakilishi wenu mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa. Msipohudhuria Baraza litasikiliza kesi upande mmoja dhidi yenu na hukumu kutolewa.
Amri hii imetolewa kwa mkono wangu na Mhuri wa Baraza hili leo tarehe 12.04.2023.

.....................................................
MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)
MULEBA

---

**IN THE DISTRICT COURT OF URAMBO AT URAMBO**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.02/2023**
**In the Matter of the Estate of the Late:**

**ERICA SIZYA NDUDU**

**AND**

**In the Matter of Application for letter of Administration by MUKULU IDDI NDUDU**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75)**

All person claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see proceeding if they think fit before the grant of probate (or letters of administration) is made to the above named petitioner.

Objection to the grant should be filed on or before the 17th May, 2023.

Dated at 13th April, 2023.

DISTRICT COURT SEAL URAMBO TANZANIA

SENIOR RESIDENT MAGISTRATE
RESIDENT MAGISTRATE I/C
URAMBO.

## KUPOTEA KWA VYETI



**LINDAIMANI RONALD ULOMI**

Anatangaza kupotelewa na cheti cha chuo cha **ASTASHAHADA(DIPLOMA OF DEVELOPMENT PLANNING)** kilichotolewa na Chuo cha Mipango Mwanza REG NO **IRDP-LZC/DDP/18 /2075** na Cheti cha (FORM FOUR ACADEMIC CERTIFICATE) REG **NO S 5202/0042** Mwaka 2016
Yeyote atakaye kiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa polisi: **MZN/RB/7534/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SIMON JAMES KIWALE** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **MITSUBISHI FUSO** yenye namba za usajili **T459 DTF** LENYE CHASES NAMBA: **FK618K521903** ENJINI NAMBA: **6DZ803ED.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa polisi. Taarifa ya polisi RB. Namba **IRI/IRI/RB/133722/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA TREKTA

**BATULI ABDLALAH MYOVELA** anatangaza kupotelewa na kadi ya **TRETKTA AINA YA FIAT** yenye namba za usajili **T 110 ALP** LENYE CHASES NAMBA: **467223 ENJINI** NAMBA: **34503** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa polisi. Taarifa ya polisi RB. Namba **IRI/IRI/RB/132750/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJ

**CLARA PATRICK MBINDA** anatangaza kupotelewa na kadi ya **BAJAJ** yenye namba za usajili **MC 106 DTY** YENYE CHASES NAMBA: **MD6M14PA5P402877.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa polisi. Taarifa ya polisi RB. Namba **IRI/IRI/RB/134568/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ALEX PAULO NASILIMIKA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 827 AWB.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **MKB/RB/459/2023.**

---

**THE REGISTRATION OF DOCUMENTS ACT**
**(CAP. 117)**
**CHANGE OF NAME BY DEEDPOLL**

**BY THIS DEED, I THERESIA SWEDI JOHN** a citizen of Tanzania, **DO HEREBY** wholly, absolutely and utterly renounce, relinquish and abandon the use of my former name of **THERESIA JOHN SUED** as it can be seen in my Parastatals Pensions Fund and adopt as from the date of this deed poll and in substitution of my former name, the name of **THERESIA SWEDI JOHN** as it appears in my National Identity Card No. **1960817-14129-0000-11.** For the purpose of evidence of such determination, I, hereby DECLARE that I shall at all times hereinafter in all records, deed, documents and other writings and in all action, suits and proceedings as well as in all Public and Private dealings and transactions and creations whatsoever use and subscribe the said name of **THERESIA SWEDI JOHN** as my name in lieu and in substitution for my former name of **THERESIA JOHN SUED. AND I HEREBY** expressly authorize and require all and every person and whatsoever at all times the date hereof to designated, describe and address me by the adopted name of **THERESIA SWEDI JOHN. IN WITNESS WHEREOF I** set my hand at Dar es salaam, and I hereon substitute my old name of **THERESIA JOHN SUED** by new name of **THERESIA SWEDI JOHN.**

SIGNED and DELIVERED by the said THERESIA SWEDI JOHN who is known to me personally/identified to me by ............ the latter being known to me personally in my presence this 04 day of 04 ...2023 } ............ DEPONENT



BEFORE:
Signature: ............
Name: ............
Postal address: ............
............
Qualification: ADVOCATE

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MOHAMMED ENTERPRISES (T) LTD.** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya Boxer yenye namba za usajili **MC 653.** YENYE CHASES NAMBA: **MD2A21BX1LWF89931** ENJINI NAMBA: **PFXWLF15106** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa polisi Taarifa ya polisi RB. Namba **IRI/IRI/RB/132865/2023**

---

**FOMU MIRATHI - 2**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya TEMEKE**

**Kituo cha Jumuishi Mkoa wa Dar es salaam**

**Usimamizi wa mirathi Na. 618 /2023**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU MWECHANDE MSHAM WA MPONDA**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOTOLEWA NA MARIAM MWINCHANDE**

**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 03 Mwezi 05 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo tarehe 20 Mwezi 04 Mwaka 2023.

HAKIMU

---

*Uza,*
*Chenye Thamani Kubwa Kwa*
*Kutangaza Nasi*
*Kwa Bei Poa*
*Tupigie 0745 700 710.*

**OFISI ZA MATANGAZO**

**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**

**MOB: +255 - 745 700 710.**

**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Maelfu wakimbia Khartoum, makombora, risasi zikirindima

**KHARTOUM,** Sudan

MAELFU ya raia wameukimbia mji mkuu wa Sudan na mataifa ya kigeni yanajaribu kuwahamisha raia wao, wakati mapigano makali yakiendelea kwa siku ya sita.

Vyanzo mbalimbali kutoka mji mkuu wa Sudan wa Khartoum, viliripoti kuwa watu walionekana wakikimbia kutoka eneo hilo kwa kutumia magari na kwa miguu.

Watu hao walikuwa wakimiminika barabarani jumatano asubuhi, huku milio ya risasi na milipuko ikitikisa jiji hilo lililo katika makutano ya mito miwili ya Nile.

Maofisa wa Japan na Tanzania walisema wanafikiria kufanya mpango wa kuwahamisha raia wao.

Msafara huo unafuatia kushindwa kwa usitishaji mapigano wa siku ya Jumanne kati ya pande zinazozozana.

Wanajeshi wa Sudan na Wanamgambo wa RSF walikuwa wamekubaliana kusitisha mapigano kwa saa 24 siku ya Jumanne, lakini mapatano hayo yalishindikana.

Usitishaji mpya wa mapigano kwa muda sawa ulitolewa na RSF juzi.

Jeshi lilisema litatii makubaliano hayo, lakini milio ya risasi bado ilisikika katika mji mkuu.

**Mohammed Alamin, mwandishi wa habari aliyeko Khartoum, aliiambia redio ya BBC Focus on Africa kwamba milio ya risasi haikuacha, licha ya madai ya kusitisha mapigano.**

Moshi ulionekana kwenye eneo la makao makuu ya jeshi katikati mwa jiji, ambako mapigano mengi kati ya makundi hasimu ya kijeshi yamejikita.

Mohammed Alamin, mwandishi wa habari aliyeko Khartoum, aliiambia redio ya BBC Focus on Africa kwamba milio ya risasi haikuacha, licha ya madai ya kusitisha mapigano.

"Inatisha sana pande zote zinazopigana zinafyatua risasi ovyo kila mahali," alisema.

"Niliona, mimi mwenyewe, mamia ya watu wakienda nje ya Khartoum, wakikimbilia katika majimbo jirani." Aliongeza.

Baadhi ya raia hawakujua kilichokuwa kikitokea, huku wengine wakielekeza hasira zao pande zote mbili zinazohasimiana.

"Kimsingi watu wanafikiri kwamba vita hivi ni dhidi yao," alisisitiza Alamin.

Pia alisema kuwa tatizo moja la kutekeleza usitishaji mapigano linaweza kuwa ni vikosi vilivyogawanyika katika jiji hilo.

"Kuna aina ya utengano kati ya askari hawa, wanapigana katika maeneo tofauti na mawasiliano hafifu," alisema. Mapigano hayo kwa sasa yanahusisha zaidi urushaji wa makombora na si mashambulizi ya mabomu ya angani.

Jeshi la Sudan lilisema kuwa wanajeshi 177 wa Misri, ambao walikuwa wamekamatwa na kikundi cha jeshi wameokolewa juzi.

Kikundi hicho kilisafirishwa kwa ndege nje ya Sudan kwa ndege nne za kijeshi la Misri.

Wanajeshi hao walikuwa wamekamatwa na kikundi cha kijeshi cha RSF Jumamosi walipokuwa katika mazoezi ya pamoja ya kijeshi na jeshi la Sudan.

Hata hivyo, jeshi la Misri halikutangaza kuhusu uokoaji huo, lakini awali lilisema kuwa linashirikiana na mamlaka za Sudan ili kuwawezesha wanajeshi hao kurejea nyumbani.

Katika hatua nyingine, wanadiplomasia wa kigeni wamekuwa wakishambuliwa na baadhi ya wafanyakazi wa misaada wameripotiwa kujeruhiwa katika ghasia hizo. **BBC**



Raia wa Sudan akibeba baadhi ya vitu vyake wakati akikimbia mapigano katika jiji la Khartoum jana. **PICHA: AFP**

## Museven, wabunge kujadili muswada mapenzi ya jinsia moja

**KAMPALA,** Uganda

RAIS wa Uganda Yoweri Museveni, anatazamiwa kukutana na wabunge wa chama tawala cha National Resistance Movement (NRM) jana kujadili muswada tata wa kupinga mapenzi ya jinsia moja uliopitishwa na bunge mwezi uliopita.

Mkutano huo umefanyika katika Ikulu ya Entebbe, kwa mujibu wa taarifa ya mwenyekiti wa kikao cha wabunge wa NRM, Denis Obua.

Wabunge wote wanatakiwa kupima Covid-19 kabla ya mkutano, tovuti ya serikali ya New Vision iliripoti.

Muswada huo, ambao vyombo vya habari vya ndani vilisema kuwa Rais Museveni huenda akatia saini kuwa sheria, utaharamisha mtu yeyote anayejihusisha na vitendo vya mapenzi ya jinsia moja.

Muswada huo unatoa adhabu ya kifungo cha miaka 20 jela na hukumu ya kifo kwa watu waliopatikana na hatia ya kuhusika na mapenzi ya jinsia moja.

Sheria iliyopendekezwa imevuta hisia tofauti kimataifa, huku Marekani ikitishia kuiwekea Uganda vikwazo iwapo muswada huo utapitishwa kuwa sheria. **BBC**

## Ujerumani yakumbwa na migomo

**BERLIN,** Ujerumani

WAFANYAKAZI katika viwanja kadhaa vya ndege nchini Ujerumani wamefanya mgomo jana kama sehemu ya kushinikiza nyongeza za mishahara katika sekta ya umma.

Migomo katika viwanja vya Dusseldorf, Hamburg na Cologne imepangwa kufanyika jana na leo, wakati wafanyakazi katika uwanja wa Stuttgart wakitarajiwa kugoma kesho.

Mgomo huo umeathiri usalama wa safari za ndege, abiria na ukaguzi wa bidhaa, pamoja na nafasi nyingine za utoaji huduma.

Chama cha viwanja vya ndege ADV kimekadiria kuwa karibu safari 700 zimefutwa hatua itakayowaathiri karibu watu 100,000.

Chama cha wafanyakazi Ujerumani Verdi na Chama cha Makampuni ya Usalama wa Anga Ujerumani wanafanya mazungumzo kuhusu marupurupu ya zamu za usiku, mwisho wa wiki na wakati wa siku kuu.

Migomo pia imepangwa kufanywa na wafanyakazi wa Kampuni ya treni ya Deutsche Bahn leo. **DW**

## DRC haitakaa mezani na M23

**NEWYORK,** Marekani

BALOZI wa Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Congo katika Umoja wa Mataifa, amesema kuwa serikali yake haiwezi kufanya mazungumzo na kikundi cha waasi wa M23, kwa sababu hakuna nchi yoyote duniani ambayo imewahi kuzungumza na 'magaidi.

Balozi Georges Nzongola-Ntalaja, aliyasema hayo katika kikao na Baraza kuu la usalama la Umoja wa Mataifa, kilichofanyika usiku wa Jumatano.

Kikao hicho kilitaka kufahamu hali ya mambo katika eneo la maziwa makuu, husussan katika mashariki mwa DRC.

Katika hotuba yake, balozi wa Congo aliishutumu Rwanda kuwa chanzo cha matatizo ya kiusalama mashariki mwa nchi yake.

Akizungumza katika kikao hicho, Balozi wa Rwanda Claver Gatete pia aliishutumu DRC kuwa kikwazo cha mpango wa amani mashariki mwa nchi hiyo, kwa kukataa kufanya mazungumzo na kuwaunga mkono waasi wa kundi la FDLR wanaoipinga serikali ya Rwanda.

Balozi Gatete alisema suala la M23 kukubali kujiondoa kwenye maeneo iliyokuwa imeyateka mashariki mwa DRC ambayo kwa sasa yamo mikononi mwa jeshi la kikanda.

"Inaonyesha kuwa M23 wako tayari kutekeleza makubaliano ya amani ya wakuu wa nchi yaliyofikiwa Luanda na Nairobi," alisema.

DRC imekuwa ikikabiliwa na mzozo ambapo jeshi la nchi hiyo, FARDC, linapambana na wapiganaji wa M23, ambao serikali inasema wanaungwa mkono na Rwanda. **BBC**

# SINGIDA BS HESABU KALI IKIWAKARIBISHA YANGA

Saada Akida na Hadija Mngwai

KATIKA kuhakikisha inapata ushindi na kusonga mbele katika mashindano ya Kombe la FA, Kocha Mkuu wa Singida Big Stars, Hans van Pluijm, amesema anakiandaa vyema kikosi chake ili kupata matokeo mazuri kwenye mechi mbili watakazocheza dhidi ya Yanga hivi karibuni.

Singida Big Stars itakutana na Yanga mara mbili ndani ya wiki moja, itacheza mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara ifikapo Mei 3, mwaka huu na siku tatu baadaye watavaana katika mechi ya hatua ya nusu fainali ya Kombe la FA (ASFC).

Mechi zote hizo, Singida Big Stars itakuwa kwenye Uwanja wake wa CCM, Liti uliopo mkoani Singida ikiwakaribisha mabingwa hao watetezi, Yanga.

**Akizungumza na Nipashe jana, Pluijm alisema rasmi michezo hiyo miwili imepangwa kufanyika mapema Mei, hivyo hana muda wa kupoteza zaidi ya kukiimarisha kikosi chake.**

Pulijm alisema wanatumia muda huu ambao Yanga wana majukumu ya kimataifa kufanyia kazi makosa yaliyopo katika kikosi chake huku akiendelea kuwasoma wapinzani kwa kuangalia video za mechi zilizopita ikiwamo ile waliyocheza Jumapili iliyopita dhidi ya Simba.

"Ndani ya Mei tunakutana na Yanga mara mbili, kwanza tunacheza nao katika ligi na baada ya siku tatu tunakutana nao tena katika mchezo wa nusu fainali FA, mechi zote ni muhimu kushinda ili kuendelea kusonga mbele," alisema Pluijm na kuongeza:

Katika ligi tunahitaji pointi tatu muhimu zitakazotupa nafasi ya kuendelea kubaki katika nafasi ya tatu ya msimamo, tunakuja kukutana nao katika nusu faili ya Shirikisho la Azam, hii mechi muhimu kwa sababu malengo yetu ni kucheza fainali," alisema Pulijm.

Kocha huyo alisisitiza wanachezaji wanatakiwa kuongeza umakini na kucheza mechi zote mbili kwa tahadhari kubwa ili kufikia malengo yao.

Naye Kocha wa viungo wa timu hiyo, Mussa Hamisi, aliiambia gazeti hili wameanza programu maalumu ya gym ili kuwajenga zaidi nyota wao kuelekea michezo hiyo itakayokuwa na ushindani.

"Tunafanya mazoezi ya gym kwa sababu tumeona mechi ya Yanga ipo mbali, tumeona tufanye mazoezi haya ili kuwaweka sawa wachezaji. Kuna faida tatu za gym, kwanza kuzuia majeruhi wakati wachezaji wakiwa na nguvu hivyo kunakuwa na nafasi ndogo ya kupata majeruhi, pili kupata usawa unapokuwa na mpira pia vile vile inasaidia kuweka vitu kadhaa vizuri ikiwamp kasi," alisema Hamisi.



Wachezaji wa Geita Gold Queens FC wakifurahia bao katika mechi ya robo fainali ya Ligi ya Wanawake Daraja la Kwanza dhidi ya Masala Queens ya Dar es Salaam iliyochezwa kwenye Uwanja wa Nyamagana, Mwanza juzi. Geita Gold Queens ilipata ushindi wa mabao 4-1. **PICHA: TFF**

## Simba yaambulia milioni 188.9

Na Adam Fungamwango

MCHEZO wa Ligi Kuu Tanzania Bara kati ya watani wa jadi, Simba na Yanga uliochezwa Jumapili iliyopita kwenye Uwanja wa Banjamin Mkapa, Dar es Salaam umeingiza Sh. milioni 410.6 huku wenyeji Wekundu wa Msimbazi wakipata Sh. milioni 188.9/.

Taarifa iliyotolewa na Ofisa Habari na Mawasiliano wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Clifford Ndimbo, imesema kiasi hicho cha fedha kimetokana na mashabiki 53,569, waliolipa tiketi kushuhudia mtanange huo uliomalizika kwa Simba kupata ushindi wa mabao 2-0.

Ndimbo (pichani) alisema kiasi cha Sh. milioni 47.2 kilikwenda kwa wamiliki wa uwanja, Sh. milioni 62 zililipwa kodi ya mapato, gharama za tiketi zilikuwa ni Sh. milioni 22.5, TFF ilipata Sh. milioni 12.5, DRFA Sh. milioni 18.8 na Bodi ya Ligi ilipata Sh. milioni 25.1.

Aliongeza mashabiki 340 waliingia kwenye eneo la VIP A wakilipa kiasi cha Sh. 30,000 kila mmoja, eneo la VIP B liliingiza watu 4,160 kwa kiingilio cha Sh. 20,000 ambapo zilikusanywa Sh. milioni 83.2, VIP C waliingia watazamaji 2,004 kwa kiingilio cha Sh. 15,000 zikapatikana Sh. milioni 30.06 huku waliokaa eneo la jukwaa la rangi ya machungwa walikuwa ni watazamaji 10,372.

Mabao ya Simba katika mechi hiyo ya raundi ya 26 ya mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Tanzania Bara yalifungwa na Henock Inonga na Kibu Denis, yote yakifungwa kipindi cha kwanza.



# JKT Queens yarudi kileleni Ligi Kuu Wanawake

Na Adam Fungamwango

JKT Queens imerejea tena kileleni katika Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania baada ya ushindi wa bao 1-0 waliopata dhidi ya Amani Queens kwenye mechi ya ligi hiyo iliyochezwa kwenye Uwanja wa Meja Jenerali Isamuhyo, Dar es Salaam juzi jioni.

Ushindi huo umeendelea kunogesha mbio za ubingwa wa ligi hiyo inayoshirikisha timu 10 kutokana na kutofautiana pointi chache kwa timu tatu zilizoko juu katika msimamo.

Kabla ya mechi hiyo ilienguliwa kwa muda wa mabingwa watetezi, Simba Queens ambao Jumanne waliichapa Mkwawa Queens mabao 4-0, mechi iliyochezwa kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam.

Maafande hao sasa wamefikisha jumla ya pointi 34 wakiwa wamecheza mechi 14, kushinda 10, sare nne, ikiendelea kuwa timu pekee ambayo haijapoteza mechi yoyote mpaka sasa, na mabao yake 32 ya kufunga.

Simba Queens imezidiwa pointi moja tu na JKT Queens, ikiwa na pointi 33, ikicheza mechi 14, ikishinda michezo 10, sare tatu na kupoteza mechi moja, ikiwa ndiyo iliyofunga mabao mengi zaidi kwenye ligi hiyo, ikipachika magoli 44 mpaka sasa.

Yanga Princess ambayo ilisajili wageni wengi msimu huu na mapema ikionekana itakuwa kwenye vita ya ubingwa, imeshapoteza mwelekeo na sasa inapambana kuweka heshima kwa kushinda michezo yake iliyobakia.

Kila timu imebakisha mechi nne tu kila moja ili kumaliza msimu huu, huku kila moja ikiwa makini kutopoteza mechi yoyote ile itakayosababisha ikose ubingwa.

Mechi nyingine ya Ligi Kuu ya Wanawake iliyochezwa kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid, Arusha, The Tigers Queens, ikiwa nyumbani ililazimishwa sare ya mabao 3-3 dhidi ya Ceasiaa Queens kutoka mkoani Ruvuma.

Matokeo yamewafanya wageni kukaa katika nafasi ya saba wakiwa na pointi 18 kibindoni huku wenyeji kufikisha pointi nane, ikiwa kwenye nafasi ya nane.

Bingwa wa ligi hiyo ataiwakilisha Tanzania Bara katika mashindano ya Afrika Mashariki na Kati (CECAFA), ili kusaka tiketi ya kushiriki fainali za Ligi ya Mabingwa Afrika zitakazofanyika nchini Ivory Coasta baadaye mwaka huu.

## ZISIKUPITE

### HAALAND, CITY SAFI

MANCHESTER City inajiandaa kumpa mshambuliaji wa Norway, Erling Haaland mkataba mpya ambao utaondoa kipengele cha kuuzwa kwa pauni milioni 150 katika mkataba wa sasa wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22. ***(Athletic)***

### POCHETTINO NA CHELSEA

CHELSEA imeamua kutomfuatilia kocha wa zamani wa Hispania, Luis Enrique na badala yake itaelekeza nguvu zake kwa kocha wa zamani wa Paris St-Germain, Mauricio Pochettino. ***(Telegraph)***

### YAMTAKA POCHETTINO

UAMUZI huo wa Chelsea wa kumkataa Luis Enrique utafungua fursa kwa Tottenham Hotspur kumpa mikoba Mhispania huyo mwenye umri wa miaka 52, kumrithi mikoba ya Antonio Conte. ***(Express)***

### FRIMPONG ATAKIWA UNITED

KLABU ya Manchester United ina nia ya kumsajili beki wa kulia wa Uholanzi na Bayer Leverkusen, Jeremie Frimpong mwenye umri wamiaka 22, huku United ikiwa tayari kuwatoa Aaron Wan-Bissaka mwenye umri wamiaka 25 na Diogo Dalot wa Ureno mwenye miaka 24. ***(Mail)***

### BARCA YAMWAZA MESSI

BARCELONA haitaweza kumsajili mshambuliaji wa Argentina, Lionel Messi, 35, kutoka Paris St-Germain kutokana na hali yao ya sasa ya kifedha, amesema rais wa LaLiga, Javier Tebas. ***(Goal)***

### FANSECA KUMRITHI MOYES

WEST Ham imembainisha Paulo Fonseca wa Lille kama mbadala wa David Moyes, ambaye huenda akaachana na klabu hiyo mwishoni mwa msimu huu. ***(Guardian)***

### ARSENAL KUMUUZA BALOGUN

ARSENAL inaweza kumuuza mshambuliaji wa England wa Chini ya miaka 21, Folarin Balogun anayecheza kwa mkopo katika klabu ya Reims ya Ufaransa msimu huu - kwenda RB Leipzig msimu wa joto ili kusaidia kufadhili uhamisho wa pauni milioni 100 kumnunua kiungo wa kati wa West Ham na England, Declan Rice, 24. ***(Metro)***

### BENZEMA MAMBO MAZURI

MSHAMBULIAJI wa Real Madrid na Ufaransa, Karim Benzema, 35, ameongeza mkataba wa mwaka mmoja, na kumbakiza katika klabu hiyo ya Hispania hadi mwaka 2024. ***(Mirror)***

### LEAO: SIONDOKI MILAN

WINGA wa AC Milan, Rafael Leao, 23, amethibitisha kuwa anataka kubakia San Siro licha ya kuripotiwa kutakiwa na Manchester City. ***(Manchester Evening News)***

### RABIOT ANUKIA LIVERPOOL

LIVERPOOL iko tayari kumsajili kiungo wa kati, Adrien Rabiot ambaye atakuwa mchezaji huru mwishoni mwa msimu huu kule Juventus. ***(Liverpool Echo)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# GUARDIOLA AFURAHIA KIWANGO MAN CITY

**●●● Hata hivyo kocha huyo analia tatizo la uchovu linawaumiza nyota wake...**

**MUNICH,** Ujerumani

PEP Guardiola amesema licha ya uchovu Manchester City ilionesha iko imara wakati walipotinga nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa ushindi wa jumla wa 4-1 dhidi ya Bayern Munich, Jumatano.

**Siku nane baada ya kushinda mechi ya kwanza ya mabao 3-0 kwenye Uwanja wa Etihad, mabingwa hao wa Ligi Kuu ya England walitoka sare ya 1-1 kwenye Uwanja wa Allianz Arena na sasa watawakabili Real Madrid kwenye nusu fainali.**

Erling Haaland alikosa penalti kipindi cha kwanza, lakini alifunga bao lake la 48 msimu huu baada ya mapumziko na kuiweka City mbele usiku huo.

Joshua Kimmich aliinyima City ushindi wa 11 mfululizo baada ya kupata penalti ambayo ilifungwa na Manuel Akanji.

City wanawinda mataji matatu msimu huu Ligi ya Mabingwa Ulaya, Ligi Kuu ya England na FA baada ya kutinga nusu fainali kwa mara ya tatu mfululizo kwenye michuano hiyo ya Ulaya.

Guardiola baada ya mchezo huo aliiambia BT Sport: "Tulitatizika katika kipindi cha kwanza. Dayot Upamecano alivunja safu zote chini ya upande wetu wa kushoto na tukapambana na Kingsley Coman.

"Tulikuwa na bahati kabla ya kukosa penalti, walipata nafasi moja au mbili na lolote lingeweza kutokea lakini tulijilinda vyema.

"Umaliziaji kutoka kwa Erling ulikuwa mzuri sana. Yeye ni mchanga sana. Uzoefu tulionao katika mashindano haya, wachezaji wanataka kufanya vizuri. Kipindi cha pili kilikuwa bora zaidi tangu dakika ya kwanza."

City itamenyana na Sheffield United katika mchezo wa nusu fainali ya Kombe la FA Jumamosi na Guardiola ana wasiwasi kuwa uchovu utakuwa tatizo.

Aliongeza: "Tumechoka. Sijui jinsi tunavyopata nafuu kucheza dhidi ya Sheffield United katika nusu fainali ya Kombe la FA."

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,104,5
MECHI KALI
ARSENAL
VERSUS
SOUTHAMPTON
1 | 1.21
X | 5.73
2 | 11.64
KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom m-pesa
halopesa
airtel money
SEND
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# INZAGHI: INTER KUFIKA NUSU FAINALI UEFA ILIKUWA NDOTO



**MILAN,** Italia

KOCHA Mkuu wa Inter Milan, Simone Inzaghi, amekiri hapo awali alikuwa kama ndoto tu kwa timu yake kutinga nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Nerazzurri hao walijumuishwa katika kile kilichochukuliwa 'kundi la kifo' mapema katika mchuano huo walipowekwa pamoja na Bayern Munich na Barcelona, na hivyo kufanikiwa kuwa washindi wa pili mbele ya wababe hao wa LaLiga.

Inter iliishinda Benfica kwa jumla ya mabao 5-3 baada ya sare ya 3-3 kwenye dimba la San Siro katika mechi ya hatua ya robo fainali ya pili iliyochezwa juzi.

Hivyo inamaanisha Inter itamenyana na wapinzani wao wa jiji moja, AC Milan katika nusu fainali kwa mara ya kwanza tangu msimu wa 2002/03.

"Kuna furaha kubwa," Inzaghi alisema baada ya mchezo. "Tulicheza mchezo mzuri dhidi ya timu ngumu.

"Tulistahili kabisa nusu fainali hii, ambayo hapo awali ilikuwa ndoto tu. Nina furaha kwa vijana na kwa maendeleo yetu. Tulianza na kundi gumu sana na Barcelona na Bayern Munich. Tulifanya kazi kila siku ili kupata uzoefu. "



## Bosi LaLiga amtaka Messi

**MADRID,** Hispania

BARCELONA "inaweza kuchukua hatua" kumsajili, Lionel Messi, lakini LaLiga haitabadilisha kanuni zake ili kusaidia hilo, kwa mujibu wa rais wa Ligi Kuu Hispania, Javier Tebas.

Tebas ameonyesha nia ya kumwona mshambuliaji huyo wa kimataifa wa Argentina akirejea Hispania.

Messi, ambaye anachukuliwa mmoja wa wachezaji bora zaidi wa wakati wote, aliondoka Barca kwa uhamisho wa bure miaka miwili iliyopita baada ya vikwazo vya kifedha kuzuia klabu hiyo kumpa mkataba mpya.

Tangu wakati huo kumekuwa na mazungumzo ya mara kwa mara kuhusu Messi kurejea kutoka Paris Saint-Germain, huku mkataba wake wa awali nchini Ufaransa ukikamilika mwishoni mwa msimu huu.

Lakini hali ya kifedha ya Barca bado haijaimarika kiasi kumrudisha namba 10 huyo.

K Tebas aliwaambia Blaugrana mwezi uliopita watalazimika kurejesha kiasi kikubwa cha ada ya uhamisho na kupunguzwa mishahara kabla ya kufanya usajili wowote.

80,144/-

SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 22/04/23 | 17:00 | Brentford FC vs Aston Villa | 2.41 | 3.20 | 2.75 |
| 02. 22/04/23 | 17:00 | Leicester City vs Wolverhampton Wanderers | 2.38 | 3.15 | 2.85 |
| 03. 22/04/23 | 19:30 | Preston North End vs Blackburn Rovers | 2.46 | 3.20 | 2.70 |
| 04. 22/04/23 | 21:00 | FC Groningen vs NEC Nijmegen | 2.75 | 3.15 | 2.44 |
| 05. 22/04/23 | 21:45 | Sampdoria Genoa vs Spezia Calcio | 2.46 | 3.10 | 2.75 |
| 06. 23/04/23 | 10:00 | Kawasaki Frontale vs Urawa Red Diamonds | 2.37 | 3.10 | 2.55 |
| 07. 23/04/23 | 13:30 | Kasimpasa Istanbul vs Konyaspor | 2.47 | 3.25 | 2.35 |
| 08. 23/04/23 | 15:30 | PSV Eindhoven vs Ajax Amsterdam | 2.32 | 3.40 | 2.75 |
| 09. 23/04/23 | 16:00 | AFC Bournemouth vs West Ham United | 2.85 | 3.15 | 2.39 |
| 10. 23/04/23 | 16:00 | AC Ajaccio vs Stade Brest 29 | 2.95 | 3.00 | 2.42 |
| 11. 23/04/23 | 18:05 | Montpellier HSC vs Stade Rennes | 2.95 | 3.30 | 2.24 |
| 12. 23/04/23 | 18:30 | Brighton & Hove Albion vs Manchester United | 2.32 | 3.45 | 2.70 |
| 13. 23/04/23 | 18:30 | Bayer Leverkusen vs RB Leipzig | 2.55 | 3.40 | 2.49 |
| 14. 23/04/23 | 20:30 | Borussia Monchengladbach vs Union Berlin | 2.28 | 3.20 | 2.95 |
| 15. 23/04/23 | 21:45 | Juventus Turin vs SSC Napoli | 2.75 | 3.05 | 2.50 |
| 16. 23/04/23 | 21:45 | Olympique Lyon vs Olympique Marseille | 2.37 | 3.45 | 2.65 |
| 17. 23/04/23 | 22:00 | Sevilla FC vs Villarreal CF | 2.85 | 3.25 | 2.34 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

IJUMAA - 21/04/2023

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 12:45 | 4048 | Western Sydney vs Wellington Phoenix | 1.79 | 3.57 | 4.04 |
| 13:00 | 5633 | Roasso Kumamoto vs JEF United Chiba | 3.04 | 3.04 | 2.21 |
| 14:35 | 2988 | Henan Jianye vs Qingdao Hainiu | 1.66 | 3.54 | 4.42 |
| 14:35 | 4003 | Chengdu Qianbao vs Shijiazhuang | 1.53 | 3.74 | 5.33 |
| 14:35 | 4523 | Shandong Luneng vs Nantong Zhiyun | 1.17 | 5.34 | 14.39 |
| 15:00 | 1708 | Keshla FK vs Kapaz | 2.00 | 3.16 | 3.52 |
| 15:00 | 4375 | Adama City FC vs Ethiopia Electricity | 1.59 | 3.57 | 5.18 |
| 15:00 | 5469 | Kolos Kovalivka vs Zorya Lugansk | 3.39 | 3.28 | 1.96 |
| 16:00 | 1155 | Polisi Tanzania vs Ihefu FC | 2.74 | 2.79 | 2.59 |
| 17:00 | 2185 | Lokomotiva Zagreb vs HNK Sibenik | 1.63 | 3.55 | 4.63 |
| 19:00 | 1983 | AEK Larnaca vs Omonia Nicosia | 1.81 | 3.49 | 4.17 |
| 19:00 | 3505 | Karabakh vs Zira | 1.24 | 5.07 | 10.34 |
| 19:00 | 3865 | Apollon Limassol vs Pafos FC | 2.80 | 3.22 | 2.43 |
| 19:00 | 5224 | Inter Youth vs Juventus Youth | 2.40 | 3.25 | 2.40 |
| 19:00 | 5501 | Wisla Plock vs Jagiellonia | 2.55 | 3.23 | 2.45 |
| 19:00 | 5836 | Chrobry Glogow vs Arka Gdynia | 3.64 | 3.48 | 1.82 |
| 19:10 | 3761 | Slaven Belupo vs NK Osijek | 2.73 | 2.99 | 2.44 |
| 19:30 | 1432 | Hamburger SV vs St. Pauli | 1.97 | 3.74 | 3.28 |
| 19:30 | 1953 | SV Darmstadt vs Karlsruher SC | 1.84 | 3.73 | 3.73 |
| 20:30 | 3882 | Wolfsberger AC vs TSV Hartberg | 1.86 | 3.39 | 3.60 |
| 20:30 | 4037 | Le Puy vs Orleans | 2.85 | 3.16 | 2.39 |
| 20:30 | 4252 | Villefranche Sur Saone vs Cholet | 1.94 | 3.37 | 3.68 |
| 20:30 | 4916 | Avranches vs Concarneau | 3.79 | 3.52 | 1.86 |
| 20:30 | 5160 | Yverdon-Sport FC vs AC Bellinzona | 1.50 | 4.01 | 5.14 |
| 20:30 | 5278 | Maritzburg Utd vs Richards Bay FC | 2.54 | 2.87 | 2.87 |
| 21:00 | 1612 | Telstar vs VVV Venlo | 2.38 | 3.28 | 2.70 |
| 21:00 | 2544 | Helmond Sport vs Heracles Almelo | 4.59 | 3.75 | 1.64 |
| 21:00 | 2590 | Dordrecht vs Jong AZ Alkmaar | 3.13 | 3.44 | 2.06 |
| 21:00 | 2658 | Almere City vs PEC Zwolle | 3.33 | 3.54 | 1.95 |
| 21:00 | 3272 | FC Eindhoven vs NAC Breda | 2.03 | 3.43 | 3.22 |
| 21:00 | 3346 | FC Volendam vs Cambuur | 1.97 | 3.46 | 3.40 |
| 21:00 | 3357 | De Graafschap vs ADO Den Haag | 1.77 | 3.75 | 3.80 |
| 21:00 | 4718 | Roda Kerkrade vs Den Bosch | 1.42 | 4.48 | 6.04 |
| 21:00 | 5104 | Budapest Honved vs Ujpest FC | 2.24 | 3.23 | 2.91 |
| 21:15 | 3310 | FC Wil vs FC Schaffhausen | 1.81 | 3.61 | 3.56 |
| 21:30 | 2790 | Reggina vs Brescia | 1.96 | 3.18 | 3.76 |
| 21:30 | 5187 | Warta Poznan vs Legia Warszawa | 3.23 | 3.08 | 2.10 |
| 21:30 | 5193 | Augsburg vs Stuttgart | 3.00 | 3.45 | 2.14 |
| 21:45 | 1134 | Shelbourne vs Dundalk FC | 2.18 | 2.98 | 3.18 |
| 21:45 | 1919 | Drogheda Utd vs Bohemians FC | 3.29 | 3.24 | 2.01 |
| 21:45 | 1933 | Cork City vs Derry City | 4.11 | 3.39 | 1.75 |
| 21:45 | 2283 | St Patricks vs Shamrock Rovers | 3.40 | 3.35 | 1.94 |
| 21:45 | 2992 | Ayr United vs Queens Park | 2.19 | 3.39 | 2.92 |
| 21:45 | 3188 | Larne vs Linfield Belfast | 1.98 | 2.98 | 3.70 |
| 21:45 | 4307 | Verona vs Bologna | 2.76 | 2.91 | 2.61 |
| 22:00 | 1492 | Espanyol vs Cadiz CF | 2.00 | 3.25 | 3.55 |
| 22:00 | 2826 | Angers vs Paris St Germain | 8.72 | 5.28 | 1.27 |
| 22:00 | 3225 | Eibar vs Zaragoza | 1.90 | 3.06 | 4.21 |
| 22:00 | 5946 | Arsenal vs Southampton | 1.21 | 5.73 | 11.64 |
| 22:15 | 4705 | Casa Pia Atletico vs Sporting Braga | 5.45 | 3.64 | 1.60 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# KIBADENI AZIPA UJANJA SIMBA, YANGA AFRIKA

**Na Hadija Mngwai**

ALIYEKUWA kocha na mchezaji wa Simba, Abdallah Kibadeni ' King ' ameitaka timu yake pamoja na watani zao, Yanga kupambana kusaka ushindi katika mechi zao za hatua ya robo fainali ya michuano ya kimataifa na kuvunja rekodi kwa mara ya kwanza katika mashindano hayo.

**Simba kesho itashuka katika mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Wydad wakati Yanga itakuwa ugenini Nigeria ikiwakabili Rivers United.**

King aliliambia gazeti hili kumbukumbu zake zinamwonyesha ni mara moja tu timu ya Simba ilifanikiwa kutinga hatua ya fainali ya Afrika lakini ilikuwa katika Kombe la Shirikisho hivyo msimu huu wajitume zaidi kuifikia au kuivunja rekodi hiyo.

"Nawapongeza Simba na Yanga katika hatua nzuri waliyoifikia ya kucheza robo fainali, hivyo wanahitaji kujipanga upya katika mechi zao zinazofuata kwa ajili ya kuhakikisha tunapita katika hatua hii na kuvunja rekodi. Simba tulifika fainali ya Kombe la CAF, wakati huo nilikuwa nafundisha Simba, tulivyocheza kwao tulishinda, tulikuja kutolewa hapa nyumbani mbele ya Rais Mwinyi (Ali Hassan), wakati huo na Stella Abdijan ya Ivory coast, hivyo tukajikuta tumepoteza kombe," alisema King.

Mkongwe huyo aliongeza anatamani kuona Simba na Yanga zinafanya vizuri zaidi msimu huu na kutimiza malengo yao ikiwa ni kuunga juhudi za Rais. Dkt Samia Suluhu Hassan.

"Ukiangalia Rais Samia anavyotoa ahadi kwa kila goli na kuwapa motisha wachezaji, pia kuna wadau wanaofuatilia na kutoa ahadi, hivyo ni wajibu wao kupambana na kuvuka hatua ya robo fainali," alisema King.



Abdallah Kibadeni ' King'.

## Yanga - Tutacheza 'kikubwa'

INATOKA UK. 24

nashukuru mchezo huo haukuzalisha majeruhi, hivyo kila mmoja yuko tayari kuipambania klabu.

Alikiri wanafahamu haitakuwa kazi rahisi kuwakabili wapinzani wao kwa sababu ya rekodi nzuri waliyonayo wanapocheza nyumbani kwao.

"Tunajua Rivers United ni timu nzuri hasa ikiwa kwao, kwa mujibu wa rekodi zinavyoonyesha hivyo, hata Wydad Casablaca ilifungwa mabao 2-1 ilipokwenda kucheza huko katika hatua za mwanzo za Ligi ya Mabingwa Afrika, ingawa ilitolewa lakini bado rekodi yake inabaki pale pale, ni wagumu mno kwao. Sisi tumeshalijua hilo, ndiyo maana ninasema tunakwenda kucheza kikubwa, na mechi nzuri zaidi itachezwa ugenini," Kamwe alisema.

Wakati Yanga inaongoza katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara ikiwa na pointi 68, Rivers United inashika nafasi ya pili kwenye Kundi B, ikiwa na pointi 23, ikizidiwa na kinara Lobi Stars yenye pointi 26.

Kundi A katika Ligi Kuu Nigeria linaongozwa na Bendel yenye pointi 28.

Mabingwa hao watetezi pia wa mashindano ya Kombe la FA watashuka dimbani wakiwa na maumivu ya kufungwa mabao 2-0 na watani zao, Simba katika mechi ya marudiano ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

## Manula azusha wasiwasi

INATOKA UKURASA 24

mashindnao haya, hatuna cha kuogopa," alisema Mangungu.

Wakati huo huo, mshambuliaji wa Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), Simon Msuva, amewaambia Simba wasicheze mpira wa kufanana na Wydad kama wanataka kupata ushindi.

"Simba wanatakiwa kuwa makini nyumbani na kutoingia katika mfumo wa Wydad Casablanca, hii timu imekuwa ikipoteza muda uwanjani na kutafuta sare hasa wakiwa ugenini. Najua kwa kiasi fulani tabia ya timu za Kiarabu ni wajanja, huwa hawatumii nguvu kubwa ugenini," alisema Msuva.

Kikosi cha Wydad Casablanca kilishawasili nchini tangu juzi kwa ajili ya mchezo huo wa kwanza wa hatua ya robo fainali.

Msuva aliwahi kuichezea Wydad Casablanca katika msimu wa 2020/22 kabla ya kutofautiana na klabu hiyo na sasa anacheza soka la kulipwa Saudi Arabia.

Michezo
Ijumaa Aprili 21, 2023
Nipashe



Guardiola afurahia kiwango City UKURASA 21

# Manula azusha wasiwasi Simba SC

## ●●● Rasmi kuikosa Wydad huku Raja Casablanca ikiuza siri za Waarabu hao...

**Na Saada Akida**

RASMI golikipa chaguo la kwanza wa Simba, Aishi Manula, ameondolewa katika mipango ya mechi za hatua ya robo fainali ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika kutokana na afya yake kutokuwa imara, imefahamika.

**Simba inatarajia kukaribisha Wydad Casablanca kutoka Morocco katika mechi ya kwanza ya hatua ya robo fainali Afrika itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.**

Manula aliumia nyonga katika mechi ya robo fainali ya michuano ya Kombe la FA iliyochezwa wiki iliyopita dhidi ya Ihefu ya Mbeya na kupelekea mchezo uliofuata, timu hizo zikikutana tena kwenye Uwanja wa Highland Estates siku tatu baadaye, kipa chaguo la tatu, Ally Salim, alisimama langoni.

Taarifa zilizopatikana jijini zinasema Manula hayuko kambini na amepewa mapumziko ya muda wa wiki mbili ili kuuguza maumivu yake.

"Manula hayuko kambini, na kama maumivu yake yataendelea, basi atafanyiwa upasuaji, kwa sasa amepewa ruhusa ya wiki mbili," kilisema chanzo chetu.

Chanzo hicho kiliongeza Kocha Mkuu wa Simba, Roberto Olivieira 'Robertinho' juzi jioni alifanya kikao na wachezaji wakongwe wa timu hiyo ili kuweka sawa sintofahamu iliyopo kuhusu nani atasimama langoni baada ya Beno Kakolanya ambaye inadaiwa haaminiki mbele ya mabosi wa klabu hiyo baada ya kubainika amesajiliwa na Singida Big Stars kwa ajili ya msimu ujao.

Chanzo chetu kilisema Kakolanya na Salim wameendelea kufanya mazoezi vizuri kwa ajili ya kuwakabili Waarabu hao nyumbani na ugenini baada ya wiki moja.

Akizungumza na Nipashe, Kakolanya, alisema anaendelea vyema na mazoezi na siku zote amekuwa akiheshimu uamuzi wa benchi la ufundi ambalo huamua nani anaaanza katika kila mchezo.

"Mimi ninafanya mazoezi kama kawaida, ila mpaka muda huu (jana mchana), sijui nani atadaka hiyo Jumamosi, tusubiri wakubwa," Kakolanya alisema.

Naye Mwenyekiti wa Simba, Murtaza Mangungu, alisema klabu yao inafahamu ubora wa Wydad Casablanca na ili kufikia malengo, watalazimika kuongeza umakini kuelekea mchezo huo.

Mangungu alisema ukaribu na urafiki waliokuwa nao na Raja Casablanca umewasaidia kuelekea mchezo huo muhimu na umewaongezea hali ya kujiamini.

"Viongozi kwa kushirikiana na benchi la ufundi tunahakikisha maandalizi yanakwenda vyema, kila idara inatakeleza majukumu hasa ya kimbinu na kiufundi, mipango yetu ni mizuri tangu mwanzo, tunaamini tutapata matokeo chanya, wachezaji wanautayari na wanauzoefu mkubwa kuelekea

INAENDELEA UKURASA 23



Wachezaji wa Yanga, Stephano Aziz Ki (kushoto) na Mudathir Yahya, wakishuka katika ndege jijini Addis Ababa, Ethiopia jana asubuhi na baadaye kupanda ndege nyingine kuelekea Nigeria kwa ajili ya kuwafuata wenyeji Rivers United katika mechi ya robo fainali ya michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika itakayochezwa keshokutwa nchini humo. **PICHA: MTANDAO**

# Yanga- Tutacheza 'kikubwa'

**Na Adam Fungamwango**

KATIKA kuhakikisha inajiweka katika nafasi nzuri ya kusonga mbele, Yanga imesema imejipanga kucheza 'kikubwa' katika mechi ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya wenyeji Rivers United itakayochezwa keshokutwa kwenye Uwanja wa Godswill Akpabio, Nigeria.

Kikosi cha Yanga chenye wachezaji 24, kilichoweka kambi fupi jijini Lagos, leo asubuhi kilitarajia kuanza safari ya kuelekea katika Mji wa Uru tayari kwa mtanange huo.

Ofisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe, alisema wanajua mechi hiyo itakuwa ngumu, lakini wataicheza kikubwa ili kufanya mchezo wa marudiano utakaochezwa hapa nchini wiki ijayo kuwa rahisi.

Kamwe alisema Yanga inajipanga kuhakikisha inapata ushindi na kujiondoa na janga la kufungwa idadi kubwa ya mabao ili kujiweka kwenye nafasi salama ya kuwania kusonga mbele.

"Watanzania wengi tunaamini timu zikija kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, kuna asilimia kubwa ya kushinda, lakini siku zote wakati mwingine mpira hauko hivyo, katika mechi hizi za mtoano kama hautocheza vizuri ugenini bado utakuwa na matatizo ukicheza nyumbani, sisi Yanga hatutamani kufikia huko, yaani tuwe na mlima wa kusawazisha mabao matano hapa,"alisema Kamwe.

Ofisa huyo alisema wachezaji wote waliocheza mechi ya 'dabi' wako vizuri na wa-

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >